HABARI KITAIFA



Mwalimu wa darasa la kwanza Shule ya Msingi Mayila iliyopo Kata ya Muhungula, Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, Jediva Fedelisi, akiendelea kusahihisha madaftari ya wanafunzi wa darasa la kwanza waliopanga mstari baada ya kufunguliwa kwa shule nchini, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# JPM, Nyusi wazindua ujenzi hospitali Chato

**Na Christina Mwakangale**

RAIS John Magufuli pamoja na Rais Filipe Nyusi wa Msumbiji, wameweka jiwe la msingi la ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda-Chato, mkoani Geita, inayotarajiwa kuhudumia takribani watu milioni 14, itakapokamilika.

Akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi, Rais Magufuli alisema ushirikiano baina ya nchi hizo mbili umeendelea kuimarika tangu waasisi wa mataifa hayo, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Samora Machel.

"Undugu wa Tanzania na Msumbiji utaendelea kuwapo leo, kesho na maisha yote. Watanzania tuendelee kufanya biashara kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu na kulinda usalama kwa ajili ya nchi zetu mbili," alisema Rais Magufuli.

Pia Rais Magufuli alimshukuru Rais Nyusi kwa kumtembelea Chato na kuongeza kuwa, nchi hizo zina makubaliano ya kushirikiana katika mambo mbalimbali ikiwamo biashara.

"Kuna kampuni za Msumbiji zinafanya kazi hapa na kampuni za Tanzania zinafanya kazi Msumbiji. Sisi wote katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), yenye zaidi ya watu milioni 450 na Mwenyekiti wetu ni mheshimiwa Filipe Nyusi," alisema Rais Magufuli.

"Biashara kati ya Tanzania na Msumbiji imeongezeka, hadi kufikia mwaka 2020 ilifikia Sh. bilioni 93.6, kuna kampuni za Msumbiji zinafanya kazi hapa na baadhi ya kampuni za Tanzania zinafanya kazi Msumbuji," alisema Rais Magufuli na kuongeza...

"Ninakushukuru Rais Nyusi kwa kuja kuweka jiwe la msingi katika hospitali hii ambayo itahudumia Watanzania, lakini sababu itakuwa kubwa itahudumia hata watu wa Msumbiji na nchi jirani."

Aliongeza kuwa Chato ina historia na Januari 9, 1967, Hayati Mwalimu Julius Nyerere alitembelea Wilaya ya Chato iliyokuwa kijiji, kufungua kiwanda cha pamba kilichojengwa kwa Sh. milioni mbili, ambacho kilikuwa na uwezo wa kuchakata marobota 20,000.

"Kwenye kiwanda hiki, Mwalimu Nyerere alichangisha fedha na yeye binafsi alichangia Sh. 2,000 kwa ajili ya kujenga Bandari ya Nyamirembe, ili iweze kusafirisha pamba kwenda Mwanza na Dar es Salaam, kwa hiyo Rais Nyusi amefika eneo ambalo alifika Mwalimu Nyerere."

Alisema kufika kwa rais huyo ni zawadi kubwa hususan kufanya uzinduzi wa hospitali hiyo ambayo ni kubwa na itakayohudumia nchi jirani.

Kadhalika, aliishukuru, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na pamoja na makandarasi na kusisitiza atawabana iwapo hospitali haitakamilika kwa wakati.

"Hospitali hii ikamilike mara moja, sababu kuweka jiwe la msingi, nimemleta rais na ameweka jiwe la msingi hapa, mmejichongea wenyewe, hospitali lazima ikamilike, sio nimeleta rais hapa siku ananipigia simu anasema vipi ile hospitali, niseme bado inajengwa."

"Nikuhakikishie Rais Nyusi, nitawabana kweli kweli Wizara ya Afya ili hospitali ikamilike mapema, mambo ya kusema awamu ya kwanza awamu ya pili, awamu ya tatu hapana, awamu zote zijengwe mara moja kukamilisha jengo," alisema Rais Magufuli.

Rais Nyusi ambaye ni Mwenyekiti wa SADC, alisema hospitali hiyo ambayo itahudumia takribani mikoa mitano na nchi jirani ni imani yake ujenzi utakamilika kama ilivyopangwa.

"Nilipiga simu juzi nikamuuliza rais uko wapi, akanijibu nipo Chato, nikasema Chato ni wapi. Akasema njoo Chato nyumbani, Nashukuru kwa kunipa nafasi kuweka jiwe la msingi na ni bahati kwetu Wanamsumbiji."

Alisema hivi sasa nchi ya Msumbiji katika mradi waliouanza unalenga kujenga hospitali kila wilaya na kwamba hospitali ya Kanda ya Chato ni mfano mzuri kwao kuwa na hospitali kama hiyo.

"Ni zawadi kwetu kutupa nafasi ya kuweka jiwe la msingi katika hospitali hii kubwa, tunatakiwa tujue watu wangapi na umbali kutoka hospitali moja hadi nyingine alisema.

Hiki tulichoona hapa ni mfano mzuri kwa sababu hii ni hospitali kubwa sana ambayo ipo karibu na mikoa mitano na nchi jirani za Kenya na Uganda naamini wataweza kuhudumiwa hapa," alifafanua Rais Nyusi.

Rais Nyusi alisema kuwa mkoa wa Geita ni tajiri kwa kuwa kuna kilimo cha mpunga, madini ya dhahabu na uvuvi wa samaki na kuwataka wananchi wa mkoa huo kufanya kazi kwa bidii.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema awamu ya kwanza ya ujenzi huo, itatumia Sh. bilioni 16 na serikali imekwishatoa Sh. bilioni 14.

Alisema ujenzi wa awamu hiyo, umekamilika kwa asilimia 90 na makabidhiano yake yanatarajiwa kufanyika, Machi, mwaka huu.

"Hospitali ya Rufani ya Kanda-Chato itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi zaidi ya milioni 14 na kwa siku itahudumia wagonjwa kati ya 700 hadi 1,000," alisema Dk. Gwajima.

# Fukuza fukuza ya mawaziri yapamba moto

**Na Waandishi Wetu**

NI mwendo wa kufukuza na kusimamisha kazi, hatua inayochukuliwa na wateule wa Rais John Magufuli tangu walipoapishwa Desemba 9, mwaka jana.

Tangu walipoapishwa wateule hao wamekuwa wakifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini na kukutana na ubadhirifu, uzembe unaofanywa na baadhi ya watendaji, hatua inayowalazimu kuwafukuza ama kuwasimamisha kazi.

Jana, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumaro, aliwavua vyeo na kuwafukuza kazi watumishi watatu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), akiwamo mhifadhi na askari wawili.

Ndumbaro aliwafukuza kazi watumishi hao kwa madai ya kuendeleza vitendo vya rushwa, uhujumu uchumi, utakatishaji fedha na ujangili, pamoja na kusababisha ongezeko la vitendo vya uharibifu kwenye pori tengefu la Mto Kilombero.

Dk. Ndumbaro alifikia uamuzi huo wakati akiongea na watumishi wa TAWA na Shirika la Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA), baada ya kutembelea bonde hilo na kukuta uharibifu ambao unatishia uhai wa chanzo hicho cha maji.

Aliagiza watumishi hao kusimamishwa kazi na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola ili waweze kuchukuliwa hatua stahiki kwa vitendo walivyofanya.

Aidha, Dk. Ndumbaro alisema serikali haiwezi kuvumilia mabaya yanayorudisha nyuma maendeleo ya nchi ikiwamo uvamizi wa kutisha katika maeneo ya hifadhi ambao ukiendelezwa unaweza kusababisha bonde kukosa maji na kukauka kwa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere, ambalo linategemea maji kutoka kwenye vyanzo hivyo.

Alisema vitendo hivyo ikiwamo ujangili umesababisha wanyama kama sheshe, viboko na tembo kutoweka kwenye hifadhi hiyo na kukosekana uaminifu kutoka kwa baadhi ya watumishi wa TAWA wanaoshirikiana na wananchi.

Kadhalika, Dk. Ndumbaro alikemea watumishi wengine wanaojihusisha na vitendo hivyo na kuwataka waache mara moja kwa sababu serikali ipo macho.

Katika hatua nyingine, Dk. Ndumbaro alimpandisha cheo Ofisa Mhifadhi daraja la II, Laurent Juma Okode, kuwa Ofisa Mhifadhi daraja la I kutokana na kuwa mwaminifu wakati akitekeleza majukumu yake ya kazi akiwa Meneja wa Pori Tengefu Kilombero.

Pia aliuomba uongozi wa mikoa na wilaya nchini kuhakikisha wanalinda mapori na mabonde tengefu yaliyopo, ili kunusuru uharibifu.

Alisema serikali inatarajia kuweka mipaka mipya ifikapo Agosti mwaka huu kwenye bonde la mto Kilombero ambayo itaondoa mgogoro baina ya wananchi waliovamia hifadhi na mamlaka za uhifadhi.

Alisema vijiji 41 vimetambuliwa baada ya kuwa na mikataba stahiki iliyopitishwa kwenye vikao mbalimbali ikiwamo vya baraza la madiwani huku kijiji kimoja kikikosa ushahidi wa kutambulika popote kuwa kilisajiliwa.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mabula Misungwi, aliwataja waliovuliwa vyeo hivyo kuwa ni pamoja na aliyekuwa Ofisa Mhifadhi daraja la II, Elisante Oktavia Akon, waliokuwa maaskari wawili wa uhifadhi daraja la II ambao ni Vicent Mkuki na Joshua Magesa.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, jana aliwasimamisha kazi wakuu wa shule wawili wa sekondari za Bahati Day na Muktuka katika Halmashauri ya Babati Mjini, kwa kushindwa kusimamia ujenzi wa mabweni ya shule hizo, kutumia gharama kubwa za ujenzi tofauti na mwongozo uliotolewa na serikali.

Alichukua uamuzi huo baada ya kuzitembelea shule hizo na kukuta kila shule imetumia zaidi ya Sh. milioni 80, huku ujenzi ukiwa katika hatua ya upauzi na taarifa za gharama za shule hizo zikiwa zimefanana kwa kila kitu.

Kufuatia hali hiyo, Silinde aliagiza uchunguzi wa kina ufanyike kujua fedha hizo zimetumikaje katika shule hizo na hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa watu wote waliohusika katika matumizi mabaya ya fedha. Pia, alitangaza kuvunja kamati za ujenzi katika shule hizo na kuagiza ziundwe upya, kuteuliwa kwa makaimu wakuu wa shule watakao simamia ujenzi huo, hadi pale utakapokamilika wakati uchunguzi ukiendelea.

Vilevile, Silinde alimwagiza Ofisa Elimu wa Sekondari Babati Mjini kuandika barua kwenda ofisi ya TAMISEMI ikieleza kwa nini asichukuliwe hatua za kinidhamu kwa kushindwa kusimamia miradi hiyo.

Kadhalika, alimtaka mhandisi wa halmashauri hiyo kuandika barua ya kujieleza kwa nini alitoa ushauri ambao haukuwa sahihi wa matumizi ya bei ya juu ya ujenzi tofauti na maelekezo ya serikali.

Naye Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, jana, aliagiza kusimamishwa kazi kwa makandarasi wawili wa Mbesso Construction Company Limited na Fabec Investment Limited, waliokuwa wakitekeleza mradi wa maji katika eneo la Buhigwe na Kaseke mkoani Kigoma kutokana na kushindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati.

Waziri Aweso alitoa uamuzi huo jana, akiwa mkoani Kigoma, wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maji mkoani humo kutokana na uwapo wa miradi isiyo kamilika kwa wakati. Vilevile Aweso alisema kutakuwa na mabadiliko kwenye wizara hiyo yatakayo waweka pembeni wahandisi wote wanao ihujumu Wizara ya Maji.

***Imeandaliwa na Christina Haule (Kilombero), Pendo Thomas (Kigoma) na Thobias Mwanakatwe (Dar).**

## HABARI KITAIFA

# Kamishna TRA agoma kuongeza muda mashine EFD

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Mhede, amekataa kuongeza muda kwa watumiaji wa mashine za kielektroniki (EFD), kutakiwa kuhuisha mfumo wa mashine hizo ambao mwisho ulikuwa Januari 7, mwaka huu.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Arusha, wakati wa kikao kazi cha siku tano na wakuu wa idara mbalimbali za TRA, makamishna, mameneja wa mikoa na wilaya. Alisema mfumo huo mpya wa kuhuisha mfumo wa mashine za EFD (update) utawezesha wafanyabiashara hao kutoa risiti halali na sahihi.

"Lakini kwetu sisi ni muhimu kuhakikisha mashine hizo zinatumika kwa wafanyabiashara wetu ili tufanikiwe zaidi kwenye ukusanyaji mapato," alisema Dk. Mhede.

Aliongeza kuwa awali walitoa muda wa mwezi mmoja tangu Desemba 7, mwaka jana, hadi Januari 7, mwaka huu kila mfanyabiashara awe amehuisha mfumo huo na kuwa kwenye protoko 2.1.

"Kuongeza muda tena ni sawa na kufanya mchezo, wakati sisi tunatekeleza sheria na hatuendi kinyume cha sheria na tunapochelewesha hili tunakwamisha ukusanyaji wa mapato zaidi, hivyo muda waliopewa umetosha hakuna kuongeza tena muda," alisema Dk. Mhede.

Kadhalika, alisema katika kuongeza makusanyo zaidi, alisema TRA kwa sasa wapo katika uchambuzi wa kutambua hoteli zote za kitalii zilizopo mikoani na wilayani ili waanze kutoza kodi kwa kila kitanda kwa siku.

Aliwakumbusha umuhimu wa watumishi hao kuzingatia miiko ya maadili ya kazi, kwa kukusanya kodi bila kuharibu wala kupendelea mtu yeyote ili kuondoa malalamiko yasio ya lazima.

Alitumia fursa hiyo kuwapongeza watumishi hao wa TRA kwa kukusanya kodi ya Sh. trilioni 2.088 katika kipindi cha Desemba mwaka jana, ambayo haijawahi kukusanywa tangu kuanzishwa kwa mamlaka hiyo.

Naye Naibu Kamishna Mkuu wa TRA, Msafiri Mbibo, alisema katika kikao kazi hicho watajikita zaidi kutatua changamoto wanazokumbana nazo kwenye ukusanyaji wa mapato, ili kuweka mikakati mipya kwa ajili ya kuongeza makusanyo zaidi, kuwezesha serikali kufanya kazi nyingi za miradi mbalimbali.

Awali, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu kutoka TRA, Alice Lukindo, alisema kikao hicho kinalengo la kuboresha utendaji kazi kwa watumishi hao na kutatua matatizo ya watumishi wanayokumbana nayo maeneo mbalimbali kama vile mipakani.

# Paroko anayedaiwa kubaka afunguliwa upya mashtaka

**Na Daniel Sabuni,** HAI

ALIYEKUWA Paroko wa Parokia ya Manushi Jimbo Katoliki la Moshi, Padri Erasmus Swai (44), ambaye anakabiliwa na kesi ya kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne, amefutiwa mashtaka ya awali na kufunguliwa upya.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Nkamba Mbosela, jana, aliwasilisha hoja ya kuifuta kesi hiyo na kufunguliwa upya katika Mahakama ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.Padri Swai, anadaiwa kutenda makosa hayo kwa mtoto mwenye umri wa miaka 17 ambaye ni mwanafunzi wa sekondari, mkoani Arusha.

Akiwa mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama, Thurston Kombe, anayesikiliza kesi hiyo, Mbosela aliiambia mahakama kwamba upande wa mashtaka umebaini upungufu unaotokana na masuala ya kipelelezi.

"Mheshimiwa Hakimu, kuna upungufu wa kiupelelezi umetulazimu kupeleka mbele yako ombi la kuifuta kesi hii, kurekebisha na kuifungua upya kwa makosa yale yale ili tuende sawa," alieleza Mbosela.

Akifafanua zaidi kuhusu uamuzi huo, Mbosela alidai kuwa upande wa mashtaka umepewa mamlaka ya kuomba kufuta na kufungua kesi upya, chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), Kifungu cha 98 (a), iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Mwendesha mashtaka huyo, aliendelea kudai mahakamani hapo kuwa makosa anayokabiliwa nayo (Erasmus Swai) ni ya kubaka na kumpa mimba mwanafunzi.

Kesi ya awali iliyokuwa ikimkabili padri huyo ni shauri, namba 159 la mwaka 2020. Kwa sasa limebadilishwa mashtaka na kufunguliwa upya kama kesi, namba 6 ya mwaka 2021.



Aliyekuwa Paroko wa Parokia ya Manushi Jimbo Katoliki Moshi, Padre Erasmus Swai (kushoto), ambaye ni mtuhumiwa wa kesi ya kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne, akitoka katika Mahakama ya Wilaya ya Hai akiwa na wakili wake, Moses Mahuna, baada ya kesi yake kuahirishwa jana. **PICHA: DANIEL SABUNI**

Baada ya maelezo hayo, mshtakiwa Swai, alisomewa mashtaka mapya ya kubaka na kumpa mimba mwanafunzi.

Akisoma hati ya mashtaka, Mbosela alidai kuwa Machi, mwaka jana katika hoteli ya Snow View, iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bomang'ombe, kwa nyakati tofauti Padri Swai alimbaka mwanafunzi huyo.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa, mshtakiwa alitenda makosa mawili, la kwanza ni kubaka chini ya kifungu cha 130 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 2002, na kosa la pili ni kumpa mwanafunzi ujauzito, chini ya kifungu cha 60 (a) cha Sheria za Elimu.


**MOPEH COMPANY LIMITED**
P. O. Box 590, Mob +255 (0))785 335544, +255 (0)713 639979 +255(0)755 731072
E-mail: mopehltd20@gmail.com - **Dar es Salaam – TANZANIA.**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na FINCA Microfinance Bank Ltd tunatoa muda wa siku 14 kwa mdaiwa aliyeorodheshwa kwenye jedwali hapo chini awe amelipa deni analodaiwa na benki ya FINCA pamoja na gharama za dalali, kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali aliyoweka kama dhamana ya mkopo aliokopa kwa mujibu wa mkataba husika. mnada utafanyika sehemu mali husika ilipo siku na tarehe kama itakavyotangazwa katika vipeperushi na gari la matangazo.

| JINA LA TAWI | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI |
|---|---|---|
| Kahama | Mhoja S. Mamboleo | Nyumba iliyoko Masumbwe Mkoani Geita |
| Kahama | Hanifa E. Mbubu | Kiwanja kilichopo Busoka na kiwanja kilichopo Mhungula-Kahama |
| Kahama | Rashid O Kiumba | Nyumba iliyopo Mhongolo - katika mji wa Kahama |
| Kahama | Yange Y. Gabriel | Nyumba iliyopo Manzese, Kahama |
| Kahama | Hamad M. Mhami | Vitu vya ndani alivyoweka dhamana vilivypo katika mji wa kahama |
| Kahama | Colletha J. Nambuo | Vitu vya ndani pamoja vya kwenye biashara alivyoweka dhamana vilivypo katika mji wa kahama |
| Kahama | Michael M. Daudi | Nyumba iliyoko Block A plot no. 238 Nyihongo Kahama |
| Kahama | Emanuel James Ngaganuki | Nyumba iliyoko Kiiza Kahama |
| Kahama | Musa M. Issa | Kiwanja kilichopo katika eneo la Nyanshimbi Kahama |
| Kahama | Gedion G. Shilla | Nyumba iliyopo Shunu Kaudo Kahama |
| Kahama | Khamis A. Assad | Nyumba iliyopo Isaka Kahama |
| Kahama | Said Hamoud Said | Kiwanja kilichopo Isaka Kahama |
| Kahama | Nasib A. Makaka | Kiwanja kilichopo Nyanshimbi Kahama |
| Kahama | Ramadhan S. Charles | Kiwanja kilichopo Mbulu Kahama |
| Kahama | Samson Simon Liston | Nyumba iliyopo Majengo Kahama |
| Kahama | Elias Mathias Simbila | Nyumba iliyopo Mhongolo Kahama |
| Kahama | Pagi Hassan Manyanda | Nyumba iliyopo Kagongwa Kahama |
| Kahama | Apolinary A. Muta | Kiwanja kilichopo Masumbwe |
| Geita | Jumapili A. Rajab | Nyumba iliyopo Katoro Geita |
| Geita | Butogwa Dioniz Buuyamba | Nyumba iliyopo Buseresere Geita |
| Geita | Samweli W. Mashimba | Nyumba iliyopo Mwembeni Geita |
| Geita | Justine Thomas Uronu | Nyumba iliyopo Nyankumbu Geita |
| Geita | Charles Mubarikiwa Gatuja | Nyumba iliyopo Kambarage Geita |
| Geita | Vicent Mwamba Mwagi | Nyumba iliyopo Katoro Geita |
| Geita | Christine C. Igokolo | Kiwanja kilichopo Butundwe Geita |
| Geita | Paul D. Masaga | Nyumba iliyopo Katoro Geita |
| Geita | Sabina Gadiga | Nyumba iliyopo Katoro Geita |
| Geita | Seni Nicholous Mabula | Nyumba iliyopo Geita Town |
| Geita | Juma T. Salum | Nyumba iliyopo Geita Town |
| Geita | Fabian L. Sayi | Nyumba iliyopo Geita Town |
| Geita | Sidion M. Kelege | Nyumba iliyopo Geita Town |
| Geita | Aliwakili M. Samson | Nyumba iliyopo Nyantorotoro Geita |
| Geita | Sadiki Jumanne Mzee | Nyumba iliyopo Geita Town |
| Geita | Ramadhan Nyakamwaga Mitinengo | Nyumba iliyopo Mkoani Geita |
| Geita | Josephat Y. Mashiba | Kiwanja kilichopo Kasamwa |
| Geita | Simon Lumerezi | Nyumba iliyopo Katoro Geita |
| Geita | Emanuel Hussein Kaboja | Nyumba iliyopo Geita Town |
| Geita | Simon M. Magi | Nyumba iliyopo Nyawilimilwa |
| Shinyanga | Yona N mbeke | Yumba iliyoko kwenye plot namba 82 block A iliyoko manispaa ya Tabora mkoani Tabora |
| Shinyanga | Fidelis Willibard Rugaimukamu | Yumba iliyoko kwenye plot namba 2 block B (Ld) iliyoko Tinde –Mianzini, Shinyanga |
| Shinyanga | Gikila M Salisali | Yumba iliyoko kwenye plot namba 646 block KK (Hd) iliyoko Bugweno manispaa ya Shinyanga |
| Shinyanga | Almas B Juma | Kiwanja kilichopo Ndembezi Shinyanga |
| Shinyanga | Chacha J mwirinyi | Kiwanja kwenye Plot No.117 Block C kilichopo Isikizya wilayani Uyuwi mkoani Tabora |
| Shinyanga | Sikuzani Juma Hussein | Kiwanja kwenye Plot No.44 Block Aa kilichopo mkoani Shinyanga. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena
2. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 4:30 asubuhi hadi saa 10:00 jioni
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4. Dhamana itauzwa **"kama ilivyo"**
5. Gharama za kumtoa mtu aliye kwenye nyumba/eneo linalouzwa ni za mnunuzi.

# Asimamishwa kazi tuhuma kumzaba makofi mjamzito

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MUUGUZI wa zamu katika Kituo cha Afya Mazwi, mjini hapo, amesimamishwa kazi kwa tuhuma za kumpiga makofi mjamzito aliyejifungulia sakafuni akiwa katika moja ya chumba hospitalini hapo.

Taarifa zinadai mjamzito huyo (jina linahifadhiwa), alifika katika kituo hicho cha afya saa saba usiku na kupokewa na muuguzi huyo wa zamu na kupelekwa chumba maalumu kwa ajili ya kusubiri kujifungua.

Imedaiwa kuwa muda mfupi baadaye mwanamke huyo alianza kulalamika kubanwa uchungu wa kujifungua, lakini muuguzi huyo aliyetajwa kwa jina la Valentine Kinyaga, alimwambia aendelee kusubiri.

Taarifa zinadai wakati akiendelea kusubiri na uchungu ukiendelea kuongezeka, muuguzi huyo alikuwa hayupo kwenye chumba hicho, ndipo mama huyo alipoamua kutandika khanga sakafuni na kujifungua.

Taarifa zinadai kuwa baada ya kujifungua, wanawake wenzake waliokuwa katika chumba hicho wakisubiri kupelekwa kujifungua walimwita muuguzi huyo wa zamu na kukuta amejifungulia sakafuni.

Imedaiwa kuwa muuguzi huyo alianza kumpiga makofi mama huyo, huku akimfokea kwanini amejifungulia sakafuni bila kumtaarifu ili ampeleke chumba cha kujifungulia.

Baada ya kudaiwa kumpiga alianza kumsaidia kwa kumtoa mtoto na kuendelea kumpa huduma za kitabibu. Ndugu wa mjamzito huyo waliokuwa wakimsubiri ajifungue, walitoa taarifa kwa uongozi wa hospitali hiyo, na mamlaka za juu za kiutawala wa hospitali hiyo.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbwanga, Jacob Mtalitinya, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kudai kuwa tayari wamemsimamisha kazi muguuzi huyo, ili kupisha uchunguzi wa tukio hilo.



Diwani wa Kata ya Liwale Mjini mkoani Lindi, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale mkoani humo, Mohamed Likoko, akihutubia mkutano wa hadhara mwishoni mwa wiki na kuwataka wananchi waendelee kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwili wa mtoto waokotwa ukiwa umenyofolewa nyeti

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MWILI wa mtoto mwenye umri wa miezi mitatu, umeokotwa huku viungo vyake vya siri vikiwa vimenyofolewa na kutelekezwa kwenye migomba karibu na nyumba ya mkazi mmoja wa jijini hapo.

Mwili huo uliokotwa Januari 10, mwaka huu, majira ya saa 2:00 asubuhi katika Mtaa wa Lolovoni, Kata ya Sokoni 1, jijini humo.

Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Salum Hamduni, alisema kwa sasa wanafuatilia taarifa kuhusu tukio hilo la kinyama.

"Sijapata taarifa kamili kuhusu tukio hilo la mtoto kuuawa na kunyofolewa sehemu zake za siri, ngoja nifuatilie nitarudi kwako," alisema Kamanda Hamduni.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Lolovoni, Orgeness Lema, alisema kuokotwa kwa mwili wa mtoto huo ni mwendelezo wa matukio ya ukatili, dhidi ya watoto yanayofanywa na watu waliokosa hofu ya Mungu.

"Nilipigiwa simu nikiwa kanisani na nilikwenda eneo la tukio. Nimeshuhudia mwili wa mtoto ukiwa kwenye migomba kando ya nyumba, ukiwa hauna miguu yote na mikono, sehemu za siri zikiwa hazipo. Niliitoa taarifa polisi na walifika na kuuchukua mwili huo," alisema Lema.

**WANANCHI WAANZISHA MSAKO**

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, serikali ya mtaa kwa kushirikiana na wananchi tayari imeanza msako wa kupita nyumba hadi nyumba kubaini nani aliyejifungua mtoto katika siku za hivi karibuni.

Mkazi wa eneo hilo, ambaye ni balozi wa nyumba 10 katika mtaa huo, Omari Shedafa, alisema alishuhudia mwili wa mtoto huyo ukiwa uchi wa mnyama, huku ukiwa hauna baadhi ya viungo.

Mkazi wa eneo hilo, ambaye mwili wa mtoto huyo umekutwa kando ya nyumba yake, Magdalena Shaushi, alisema alipata taarifa kwa watoto waliokuwa wakicheza kwenye migomba yake na alipofika alishuhudia mwili wa mtoto huyo na kutoa taarifa kwa balozi.

"Mimi nimeambiwa na watoto waliokuwa wakicheza, kwamba kuna mtoto ametupwa na nilipofika nilikuta mwili wa huyu mtoto. Sasa sijui ni nani amemtupa hapa kwenye nyumba yangu," alisema mkazi huyo wa Lolovoni.

Mwili wa mtoto huyo, umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, ukisubiri taratibu nyingine za kiuchunguzi.

# Simbachawene aishukia kampuni kushindwa kuleta magari

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema kampuni ya Ashok iliyopewa tenda ya kuleta magari ya Jeshi la Polisi tangu mwaka 2013 hadi sasa haijaleta magari 369.

Simbachawene alisema hayo jana, jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari alipomaliza ziara ya kutembelea vikosi vya jeshi hilo ikiwamo Bohari Kuu.

Alisema mkataba huo una miaka minane na hadi sasa haujakamilika na makubaliano ilikuwa ndani ya mwaka mmoja magari yawe yameletwa yote 777.

"Jambo moja ambalo limekuwa tatizo namna ambavyo tulipata mkataba na Ashok wa kutununulia magari 777. Magari yaliyoletwa mpaka sasa ni 497 na huu mkataba ni wa muda mrefu ingawa bado upo 'valid' tunatarajia watekeleze huo mkataba," alisema waziri.

"Hata katika magari hayo 497 yaliyoletwa, bado magari 22 yalionekana sio mazuri tukayarejesha tukiyajumlisha yote karibu magari 369 tunawadai Ashok watuletee hayo magari, sasa maelezo yamekuwa mengi," alisema.

Waziri Simbachawene alisema, amewaelekeza viongozi na atakwenda kuzungumza na Katibu Mkuu kwa ajili ya kuitisha kikao cha wadau wote kwa sababu mikataba ya serikali inahusisha taasisi nyingi akiwamo Mwanasheria wa Serikali ili wakutane kwa pamoja na kujadiliana.

Alisema baada ya kukutana watamuita mkandarasi ili awajulishe ni lini watayapata hayo magari kwa kuwa jambo hilo limekuwa ni la muda mrefu tangu mwaka 2013.

Vilevile, alisema kama kutakuwa na hatua za kuchukuliwa atazijua baada ya kukutana na wadau wa serikali waliohusika katika mkataba huo.

"Katika kipindi cha mwaka mmoja ikawa miaka nane ni dhahiri humo katikati kutakuwa na mjadala pengine mabadiliko ya hapa na pale ndio maana mkataba tunasema upo valid nataka kuingia katika jambo hili kwa kuanza na sisi watu wa serikali tukutane, tujadiliane ndipo tumuite mkandarasi aweze kuona kuna maeneo amewajibika kama kuna hatua za kuchukua basi tutachukua," alisema.

Alisema Bohari Kuu inashughulika na utunzaji na utengenezaji wa silaha pamoja na kushona sare za askari na kuisaidia serikali kupunguza gharama.

"Kuna muda sare za Jeshi la Polisi zilikuwa zinanunuliwa nje ya nchi kwa sasa wanazishona wenyewe licha ya mazingira ya kazi yao sio nzuri."

"Tunamshukuru Rais John Magufuli alitupatia Sh. milioni 666 tunajenga workshop nzuri na maeneo ya kuhifadhi na kupokea mizigo kwa hiyo ujenzi unaendelea vizuri upo kwenye asilimia 85. Kimsingi Bohari Kuu inafanya kazi vizuri changamoto ni mkoani," alisema Waziri Simbachawene.

# Lukuvi ataka usimamizi ardhi ngazi za mitaa

**Na Munir Shemweta,** SINGIDA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri nchini kusimamia ardhi kuanzia ngazi za mitaa na vijiji ili ziweze kuepuka na ujenzi holela na kurahisisha ufuatiliaji makusanyo ya kodi ya pango la ardhi.

Akizungumza wakati akikagua ofisi ya ardhi katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida, katika ziara ya siku moja kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi mkoani hapo juzi, Lukuvi alisema ni vyema wakurugenzi katika halmashauri nchini wakawapa wajibu watendaji wa mitaa na vijiji kwa barua kusimamia misingi ya ardhi yenye lengo la kusimamia sheria katika masuala ya ardhi.

Waziri Lukuvi alisema, watendaji wa mitaa na vijiji watakaokasimia mamlaka ya usimamizi ardhi katika maeneo yao hawatakuwa na jukumu la kugawa, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, bali kuangalia yanayoendelea katika mitaa yao na wakikuta ukiukwaji wowote wa ujenzi holela watakuwa na wajibu wa kusitisha.

"Ofisa ardhi katika wilaya hawezi kujua yale yanayoendelea kwenye mtaa au kijiji na hata suala la kodi mkiwatumia watendaji wa mitaa watasaidia kuwabaini wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi kirahisi," alisema.

Aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri kutengeneza majedwali maalum yenye orodha inayoonyesha kila mmiliki wa kiwanja kwa lengo la kuwawezesha watendaji wa mitaa kuwajua wamiliki katika maeneo yao.

"Kumbukumbu zote za masuala ya ardhi wajulishwe watendaji wa mitaa na vijiji ili waweze kufuatilia katika mitaa yao maana katika suala la hati za kimila tumefanya vizuri ngazi ya vijiji ila suala la hatimiliki za ardhi bado tuko nyuma maana tumeficha taarifa wilayani," alisema Lukuvi.

Alizitaka ofisi za ardhi za mikoa kutoa elimu kwa watendaji wa mitaa na vijiji ili kuwajengea ufahamu wa masuala ya ardhi na kuwawezesha kusimamia vyema masuala hayo katika maeneo yao.

Kwa mujibu wa Lukuvi, hata kama manispaa imepanga matumizi bora ya ardhi ni vyema matumizi yake yakawekwa kwenye vipande vya ngazi ya mitaa na kusisitiza kuwa kazi hiyo ni ya halmashauri kwa kuwa mitaa ni jicho lake la kutoa taarifa katika masuala mbalimbali yakiwamo ya ardhi.

Katika ziara hiyo, Lukuvi alitembelea halmashauri za Wilaya ya Singida na Ikungi na kusisitiza kuwa halmashauri ndizo zenye jukumu la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo yake na jukumu hilo siyo la maofisa ardhi.

Lukuvi alisema halmashauri zote zina wajibu wa kusimamia ardhi katika maeneo yao na ilichofanya Wizara ya Ardhi ni kuwapatia wataalamu watakaowasaidia kujua namna bora ya kutumia ardhi vizuri.



Mbunge wa Chalinze mkoani Pwani, Ridhiwani Kikwete, akitoa neno la shukrani baada ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Msata kukabidhiwa msaada wa vifaa vya shule yakiwamo mabegi na kalamu, jana, kutoka Taasisi ya Flaviana Matata Foundation. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wazazi wadaiwa chanzo kushuka ufaulu

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAZAZI na walezi wa wanafunzi wa darasa la saba wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara, wametajwa kuwa chanzo cha kushuka kiwango cha ufaulu, wakidaiwa kuwashawishi watoto wao 'kuboronga' wanapojibu maswali ili wasifaulu mtihani wa taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Changwa Mkwazu, alisema jana alipokuwa akijibu moja ya hoja kuhusu elimu na kushuka kwa kiwango cha ufaulu katika shule za halmashauri hiyo.

Alitoa maelezo katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Masasi (DCC) kilichoshirikisha wadau wakiwamo viongozi wa dini, vyama vya siasa, wazee maarufu pamoja watendaji wa serikali.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ina shule za msingi 126, lakini kiwango cha ufaulu kimeshuka kwa wanaomaliza elimu ya msingi.

Mkwazu alisema baada ya kushtushwa na hali hiyo inayojitokeza kila mwaka, halmashauri ilifanya uchunguzi kubaini chanzo cha sababu inayoporomosha viwango vya ufaulu kwa wanafunzi wa darasa la saba na kubaini kuwa wazazi wanahusika wakiwalazimisha watoto wafeli kwa madai ya kutokuwa na fedha za kuwasomesha.

Alisema walizungumza na baadhi ya wanafunzi na baadhi yao walisema wamekuwa wakikatazwa kufaulu mitihani yao na siku ya kufanya mtihani wanatakiwa wasijibu maswali kwa usahihi kama walivyoagizwa na wazazi na walezi wao.

Aliwaambia washiriki kuwa kutokana na hali hiyo halmashauri itafanya uhamasishaji kwa kukutana na wazazi na walezi ili kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza katika elimu kwa watoto wao ikiwa ni pamoja na kuwapatia haki ya kusoma na kuelimika ili kuondoa dhana potofu waliyo nayo.

# Wadau waomba ongezeko bajeti afya, elimu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAKAMU Mwenyekiti wa Baraza la Watoto Manispaa ya Shinyanga, Nancy Kasembo, ameiomba serikali kuongeza bajeti ili kupata fedha za kutatua matatizo ya sekta za afya na elimu.

Kasembo alibainisha hayo juzi kwenye mdahalo wa kujadili utekelezaji wa bajeti jumuishi katika sekta zinazomhusu mtoto moja kwa moja, ulioshirikisha maofisa maendeleo ya jamii, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, walimu, wachumi, wadau wa masuala ya watoto, jamii, na wanasiasa, ulioandaliwa na Shirika la Save the Children.

Alisema miaka ya nyuma mabaraza ya watoto yalikuwa hayashirikishwi kwenye utoaji wa mapendekezo ya bajeti hasa kwenye sekta ambazo zinamhusu mtoto ikiwamo ya afya na elimu, lakini kwa sasa wanashirikishwa na kuomba mapendekezo ambayo wanatoa kwenye bajeti hizo, lakini hayapewi kipaumbele.

"Watoto tunakabiliwa na changamoto nyingi sana hasa ukosefu wa huduma kwenye sekta za afya na elimu, mfano kwa sasa kuna tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa na wenzetu waliofaulu kuanzia kidato za kwanza wamekosa nafasi, pia hakuna madawati ya kutosha na matundu ya choo kwenye baadhi ya shule ni shida," alisema Kasembo.

"Kwenye mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2018-2019 tulitoa mapendekezo haya kwenye sekta ya elimu ili yafanyiwe kazi, lakini kama yangetekelezwa kusingekuwapo na upungufu wa vyumba vya madarasa, madawati na matundu ya choo, hivyo tunapotoa ushauri kama watoto tunaomba ufanyiwe kazi," aliongeza.

Alisema katika afya wanakabiliwa na upungufu wa vituo vya kutolea huduma za watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo kubakwa (One stop center), pamoja na madaktari wa kuwapatia huduma na kuomba suala hilo pia lifanyiwe kazi ili vituo hivyo viwepo kwenye huduma zote za kiafya.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi, alisema serikali inatamani mapendekezo yote ya bajeti yafanyiwe kazi, lakini tatizo linatokana na ufinyu wa bajeti na kutoa wito kwenye upangaji wa bajeti vitolewe vipaumbele vichache ambavyo ni muhimu ili vitekelezeke.

Mratibu wa Mradi wa Mijadala katika masuala ya uchumi na utawala wa kifedha, Alex Enock, kutoka Save the Children mkoani Shinyanga, alisema wameandaa mdahalo huo, ili wadau wajadili kwa pamoja namna ya kupanga bajeti bora ya mwaka 2021-2022 ambayo itazingatia maslahi na ustawi wa watoto.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## 'Tunasaluti' miaka 57 Mapinduzi ya Zanzibar

**LEO** ni maadhimisho ya miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar, yaliyofanyika Januari 12, 1964.

Tunawapongeza Watanzania wa Zanzibar na Pemba wanapokumbuka siku hii muhimu ya kihistoria iliyoleta uhuru.

Tunaposherehekea Mapinduzi tunatizama nyuma na kufurahia mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa nchi yetu.

Miongoni mwa malengo makubwa ya Mapinduzi ya Zanzibar yanabakia kuleta maendeleo kwa wananchi.

Ikiwa pamoja na elimu, afya, barabara, makazi na nishati ili kubadilisha maisha ya wananchi kwa kuyafanya yawe bora zaidi kutokana na ukandamizaji uliodumu kwa karne kadhaa.

Leo Watanzania tuna kila sababu ya kufurahia mafanikio miongoni mwa sekta zilizobadilisha maisha ya wananchi wetu kiuchumi hasa wanaoishi vijijini.

Tukitazama maisha ya Wazanzibari wengi tunafurahi kuwa yamekuwa bora kutokana na uwepo wa umeme.

Tunalipongeza Shirika la Umeme (ZECO) kwa kuwafikishia wananchi kwa asilimia 80 huduma hiyo.

Limesambaza nishati hiyo muhimu kutoka mijini hadi vijijini na kusaidia kuwapo kwa mabadiliko makubwa ya ukuaji wa uchumi na kupambana na umaskini miongoni mwa Watanzania. Tunawakumbuka na kuwaenzi waasisi kwa kusaidia kufanikisha ujenzi wa miundombinu ya umeme ukiwa ni pamoja na kupitisha waya baharini ili kuusafirisha umeme kwa wananchi bila kujali gharama wala usumbufu.

Ni dhahiri Wazanzibari wengi wanaoishi mijini na vijijini watakubaliana nasi kuwa juhudi za ZECO za kuvifikishia umeme vijiji 2,695 kati ya vijiji vyote 3,260 viliopo Unguja na Pemba zinastahili kushangiliwa kwa kuwa zimeakisi kikamilifu lengo la mapinduzi. Kila mmoja anazifahamu faida za umeme ambazo pamoja na kumulika na kutuondoa gizani ni nuru shuleni inayowawezesha watoto wetu kusoma bila kujali ni mchana au usiku.

Aidha, ndicho chanzo cha kuendesha mitambo kuanzia mashine ndogo vijijini zinazotumiwa na wajasiriamali kuzalisha na kubadili maisha yao na kuondokana na umaskini hadi kusukuma mitambo ya viwanda vikubwa.

Tunapoadhimisha miaka 57 ya Mapinduzi ZECO imevifikishia umeme visiwa vidogo viliopo Unguja na Pemba na nishati hiyo imebadilisha maisha ya wakazi wa sehemu hizo wakiwamo wavuvi ambao kinachoonekana ni mabadiliko makubwa ya kiuchumi. Yote hayo yanapunguza pengo la utofauti kati ya maisha ya mjini na vijijini kupunguza umaskini. Kama wazalendo na wapenda taifa letu, tuendelee kuenzi mapinduzi kwa kuendeleza hisia za upendo na uvumilivu baina yetu huku tukidumisha amani na utulivu.

Ili Watanzania tufurahie maendeleo na mafanikio kwenye sekta muhimu hasa elimu, afya, ajira, miundombinu na nishati ni lazima serikali zifanye juhudi kubwa za kufanikisha upatikanaji wa kazi (ajira). Tunahitaji kuona nafasi nyingi zaidi za kazi ili kuwapa watu wetu mapato ziwe za kujiajiri au za kuajiriwa ili wananchi wamudu maisha yao kikamilifu.


Tunahitaji kuona Serikali ya Muungano na ya Mapinduzi Zanzibar zikishirikiana na kuanzisha uwekezaji mkubwa wa bahari kuu ili uchumi wa bluu unufaishe Watanzania.

Tunapoona fahari kusherehekea Mapinduzi, tuone uchungu kuwa kwa miaka 57 hatujaweza kufanikisha uwekezaji uchumi wa bahari kuu. Ni wazi kuwa tumejenga miundombinu ya kisasa, kuzalisha umeme na kuusambaza vijijini, kujenga shule na vyuo vikuu pamoja na kuongeza wasomi, lakini hatujawezekeza kwenye bahari kuu na kuvuna kikamilifu rasilimali zilizoko.

Tunaamini ni sekta muhimu itakayoleta ajira na kuinua uchumi wa Mzanzibari na Jamhuri yetu, shime serikali zisikie hili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Acheni kuwahamasisha watoto kuboronga shuleni

**WAZAZI** na walezi ni wadau muhimu wa elimu wenye mchango mkubwa wa kuhakikisha watoto wanafanya vizuri katika masomo na mitihani, kwa ajili ya maendeleo yao ya baadaye.

Hata hivyo, kumekuwapo na madai kwamba, baadhi hushiriki kuhujumu ndoto za watoto wao kwa kuwashawishi wafanye vibaya katika mitihani ya mwisho ili wasiendelea na masomo ya sekondari.

Wanafanya hivyo ili kuwatumia katika mambo yao ikiwamo kuwaozesha na wengine kuwafanyisha kazi za kilimo na ufugaji na kukwamisha kufanikisha ndoto zao za baadaye katika elimu.

Hao wanaofanya hivyo ni wale wenye malengo mabaya kwa watoto wao, na serikali imekuwa ikiwaonya na kuwataka waache mtindo huo, lakini bado wapo ambao wanaendelea kuundeleza upotoshaji.

Juhudi zote zinazofanywa na serikali za kutoa elimu bure kuanzia chekechea hadi kidato cha nne, hawazioni, wanajali maslahi yao binafsi ambayo kimsingi hayawezi kuwasaidia watoto wao.

Mfano mmojawapo ni wazazi na walezi wa mkoani Mtwara, hasa katika wilaya za Nanyumbu na Tandahimba, ambao wanadaiwa kufurahia anguko la watoto wao kwa kuwalazimisha kufanya vibaya mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi kwa muda mrefu.

Hilo linathibitishwa na Ofisa Elimu wa Wilaya ya Nanyumbu akihojiwa na redio moja, kwamba baadhi ya wazazi wa watoto walioshindwa mtihani huo, katika Shule ya Msingi Kilimahewa walifanya sherehe kufurahia kufeli kwao.

Kitendo hicho kinatisha ustawi wa elimu kwa watoto, kwani wazazi na walezi wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwaelekeza ama kuwafundisha kuzingatia masomo, kwa ajili ya maendeleo yao ya baadaye.

Wazazi na walezi wana wajibu wa kuhamasisha watoto wao kufanya vizuri katika masomo na mitihani yao ya mwisho, lakini wanapogeuka kuanza kuwashawishi wafanye vibaya, wajue kuwa wanadidimiza elimu.

Ni jambo linaloshangaza katika karne hii kuna mzazi ama mlezi anayefurahia mtoto wake kufanya vibaya kwenye mtihani. Hiyo inaonyesha kuwa watu aina hiyo elimu si kitu chenye umuhimu kwao ndiyo maana wanahamasisha watoto wasifaulu.

Hii siyo karne ya mzazi ama mlezi kuhamasisha mtoto kubaki mbumbumbu akikaa nyumbani ili kusaidia kulima, kuvua, biashara, kuolewa au kuozeshwa kwani yote hayo hayanufaishi familia wala watoto.

Uhamasishaji wa mtoto kupenda shule ama elimu unaanzia nyumbani, kutokana na ukweli kwamba, mwalimu wa kwanza wa mtoto ni mzazi mwenyewe au mlezi. Lakini hao wote wakiwa ni maadui wa elimu, ni wazi mtoto hawezi kusoma na hata akibahatika kupelekewa shule, hawezi kuwa na maendeleo mazuri darasani, kwa kuwa hana mtu wa kumhamasisha kupenda shule.

Kimsingi, elimu bora inahitaji ushiriki wa wazazi na walezi, lakini pia jukumu lao kuhakikisha watoto wanapata elimu na siyo kuacha wahudhurie shule tu na kisha kushawishiwa kufanya vibaya katika mitihani.

Wazazi na walezi wana nafasi kubwa na wajibu wa kuhakikisha watoto wao wanahudhuria shule na kujifunza, kuwa na nidhamu ili waweze kufanya vizuri katika masomo na hatimaye watimize ndoto zao za baadaye katika elimu.

Wapo wazazi na walezi wenye shauku ya kuona watoto wao wanafanya vizuri katika masomo, lakini kuna wanaofurahia kufeli kwa watoto wao, hali inayoonyesha kuwa hawaoni umuhimu wa elimu.

Kwa ujumla mtindo huo unakwamisha maendeleo ya watoto wao kielimu, hivyo ni vyema ukatafutiwa ufumbuzi wa kudumu ili wahusika wasiendelee kuvuruga ndoto za baadaye za watoto wao kwa kuwatungia sheria ndogo ndogo za kuwabana wahusika ikibidi washtakiwe.

Ni wakati wa kutambua kuwa fedha zinazotumika katika elimu bure zinatokana na makusanyo ya kodi kutoka vyanzo mbalimbali ikiwamo wananchi wenyewe ambao ni wazazi na walezi hivyo washirikiane na serikali kufanikisha lengo jema la taifa la kuona kuwa kila mmoja anasoma.

# SUMA JKT yabanwa ujenzi kiwanda cha chaki

**Na Happy Severine,** SIMIYU

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanaidi Ali Khamis, amemtaka mkandarasi kampuni ya SUMA JKT anayejenga kiwanda cha chaki na vifungashio wilayani Maswa, mkoani Simiyu, kukamilisha mradi huo ifikapo Januari 15, 2021.

Alisema kuwa wiki moja iliyopita Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo, alitoa muda huo na kumtaka mkandarasi huyo kuzingatia agizo hilo na kutekelezwa kama inavyotakiwa.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani humo, alipotembelea ujenzi wa viwanda hivyo ambavyo vinagharimu zaidi ya Shilingi bilioni nane na kufikia asilimia 90 kabla ya kukamilika.

Baada ya kukagua mradi huo, Naibu Waziri alisema utakapokamilika utaongeza mapato ya halmashauri na wananchi watapata ajira.

Alimwelekeza mkandarasi huyo kufanya kazi usiku na mchana, kwa kuwa muda aliopewa umebaki mchache na serikali haitaongeza mwingine.

"Waziri wa TAMISEMI wiki moja iliyopita alikuja hapa na akatoa muda hadi tarehe 15, Januari 2021, niwatake SUMA JKT maagizo ya Waziri yanabaki pale pale, tena niwaombe msifike hiyo tarehe, tukabidhi hata tarehe 14, ili kiwanda kianze kufanya kazi," alisema.

"Wizara tumeanzisha hii miradi kwenye halmashauri ili kupunguza utegemezi serikali kuu, tunategemea kukamilika kwa mradi huu ajira zitaongezeka, lakini hata mapato kwenye halmashauri nayo yataongezeka," alisema.

Awali, akitoa taarifa ya mradi huo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Fredrick Segamiko, alisema ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 90 ya ujenzi wake na unagharimu zaidi ya Sh. bilioni nane.

Dk. Segamiko alisema katika mradi huo wamepokea Sh. bilioni 4.1 sawa na asilimia 49. 9 ya fedha zote za mradi na mkandarasi anaendelea na ujenzi kuhakikisha ndani ya muda aliopewa anakamilisha.

Mbunge wa jimbo hilo, Stanslaus Nyongo, aliomba serikali kutoa fedha mapema za kununulia mashine ambazo zitatumika kwenye kiwanda hicho baada ya ujenzi wake kukamilika.

# Prof. Kanywanyi kuagwa ukumbi wa Nkrumah

**Na Christina Mwakangale**

MHADHIRI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Shule Kuu ya Sheria, Profesa Josephat Kanywanyi, aliyefariki dunia juzi, anatarajia kuagwa leo katika ukumbi wa Nkrumah, chuoni hapo.

Mhadhiri wa UDSM, Shule Kuu ya Sheria, Profesa Khoti Kamanga, aliiambia Nipashe jana.

Alisema Prof. Kanywanyi ni miongoni mwa watu maarufu nchini na barani Afrika waliobobea katika sheria kwa miaka mingi.

"Tunatarajia kumuaga katika ukumbi wa Nkrumah hapa chuo kikuu leo, kuanzia majira ya saa 5: 00 asubuhi na kisha mazishi," alisema Prof. Kamanga.

Prof. Kanywanyi, aliwahi pia kushika nyadhifa serikalini na sekta binafsi, alizaliwa Novemba, mwaka 1938 na kufariki dunia usiku wa kuamkia juzi, katika Hospitali ya Kairuki alikokuwa akipata matibabu.

Kwa mujibu wa Prof. Frederick Kaijage, msemaji wa familia ya marehemu, akizungumza na moja ya chombo cha habari, Prof. Kanywanyi, atazikwa kesho katika makaburi ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Marehemu Prof. Kanywanyi aliwahi kuwa msimamizi wa nje wa Kitivo cha Sheria wa Chuo Kikuu cha Haile Selassie, nchini Ethiopia, Chuo Kikuu cha Nairobi (Kenya), Makerere (Uganda), Shule ya Sheria Zambia, Idara ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Zimbabwe na Chuo Kikuu cha nchini Swaziland, nchi ambayo kwa sasa inaitwa, Eswatini.

Pia, aliwahi kuwa mjumbe wa bodi ya wakurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na mjumbe Tume ya Huduma za Mahakama, Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani, mwaka 1993-1994.

Kadhalika, mwaka 1998-2000 alikuwa Rais wa Mahakama ya Comesa (Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika) na alikuwa Wakili wa Mahakama Kuu tangu mwaka 1978.




Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, Vita Kawawa, akichangia hoja kwenye kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Ruvuma, kilichofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea mkoani humo, jana. **PICHA: MICHAEL EMMANUEL**

# Taletale aanza kutekeleza ahadi za kampeni

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MBUNGE wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Hamis Taletale, amechimba visima viwili katika vijiji vya Diguzi na Sinyailime, Kata ya Matuli, Halmashauri ya Morogoro ikiwa ni moja ya utekelezaji wa ahadi zake.

Visima hivyo vyenye uwezo wa kutoa maji lita 20,000 kwa saa moja kila kimoja vitasaidia zaidi ya wakazi 9,000 wa vijiji hivyo.

Akizungumza baada ya kukamilisha uchimbaji wa visima hivyo, Taletale alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kuwatua ndoo kina mama.

Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha wananchi wake wanapata maendeleo kwa haraka na katika kufanikisha hayo ni muhimu kuwapo ushirikiano wa kutosha baina ya wananchi na viongozi.

"Naona maendeleo yakianza kuchipua kwa kasi sana baada ya miaka kadhaa kero za mama zetu zitapungua kwa kuwatua ndoo kichwani kwa sababu visima hivi vina uwezo wa kutoa maji lita elfu ishirini kwa saa moja kwa kila kisima," alisema Taletale.

Kadhalika alisema ofisi yake inaendelea na jitihada za kuchimba visima hivyo katika Tarafa ya Ngerengere ili wananchi waondokane na adha ya kutumia maji ya chumvi.

Wakazi wa vijiji hivyo akiwamo Shabani Danganya, alimshukuru mbunge huyo kwa kutekeleza ahadi yake hasa kutatua changamoto ya maji katika maeneo hayo ya pembezoni mwa Mkoa wa Morogoro.

Alisema kupatikana visima hivyo kutawaondolea changamoto ya kufuata maji muda mrefu na kushindwa kufanya shughuli nyingine za maendeleo.

"Visima hivi kwa kweli vimetutia moyo sana katika kuendelea kufanya shughuli zetu za maendeleo maana awali tulikuwa tunatumia muda mwingi kutafuta maji huku hali zetu za kiuchumi haziendi sawa," alisema Danganya.

# Aweso aagiza makandarasi wawili kusimamishwa

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, ameagiza kusimamishwa makandarasi wawili wa Mbesso Construction Company limited na Fabec Investment limited waliokuwa wakitekeleza mradi wa maji katika eneo la Buhigwe na Kaseke, mkoani Kigoma kutokana na kushindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati.

Alitoa uamuzi huo jana akiwa mkoani humo wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maji kutokana na uwapo wa miradi isiyo kamilika kwa wakati.

Vile vile, alisema kutakuwa na mabadiliko makubwa kwenye wizara hiyo yatakayo waweka pembeni wahandisi wote wanao ihujumu Wizara ya Maji au wasioendana na kasi katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Wizara ya Maji imekuwa ikilalamikiwa sana, hivyo ukiona umewekwa pembeni ujue ulikuwa huendani na kasi," alisema.

Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini mkoani Kigoma (RUWASA), Mathias Mwenda, alisema kwa sasa upatikanaji wa maji vijijini ni asilimia 66.

Alisema makandarasi walioshindwa kukamilisha miradi kwa wakati wamesha waandikia barua akiwamo mkandarasi wa Construction Company Limited ambaye ametekeleza mradi kwa asilimia 45.



Kazi ya ujenzi wa kingo za Daraja la Kizengi katika barabara ya Nyahua – Chaya (km 85.4), mkoani Tabora ukiendelea. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi za serikali zadaiwa mil. 339/-

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea (MANAWASA), inazidai Sh. 339,078,242.5 taasisi za serikali madeni ya maji yaliyotumiwa kuanzia Januari hadi Desemba mwaka 2020.

MANAWASA imedai kuwa deni hilo linakwamisha utendaji kazi wa mamlaka hiyo.

Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Tuntufye Mwamsojo, alisema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya MANAWASA katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Masasi (DCC).

Alisema kuanzia Januari hadi Desemba taasisi hizo hazijalipa madeni na kuwa wadaiwa sugu wa bili za maji.

Alisema ili mamlaka hiyo iweze kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma ya maji kwa wateja wake inahitaji makusanyo yafanyike kwa wakati, lakini inavyotokea baadhi ya wateja kushindwa kulipa bili mamlaka inakwama kujiendesha.

Aliwaomba wadaiwa hao kulipa bili zao ili mamlaka ipate fedha hizo zitakazosaidia utekelezaji wa malengo ya mamlaka hiyo na kujiendeshe kwa ufanisi zaidi inategemea fedha za malipo ya bili kutoka kwa wateja.

Pia, alisema mamlaka imeongeza mauzo ya maji na kusimamia makusanyo kwa kipindi cha mwaka jana na ongezeko limefikia mita za ujazo 1, 063,918.

Alisema, katika kipindi hicho cha uzalishaji wa maji kwa mji Masasi na Nachingwea ulikuwa mita za ujazo 1,341, 098 licha ya kukabiliwa na matatizo kadhaa ikiwamo ya uhaba wa vitendea kazi kama vyombo vya usafiri kuvifikia na kuvisimamia, pamoja na kufuatilia miradi ya maji katika eneo hilo

Alitaja tatizo lingine ni kutolipwa kwa madeni ya nyuma kutoka taasisi za umma, ukosefu wa mitambo ya ujenzi katika wilaya za Masasi na Nachingwea kwa ajili ya matengenezo ya mabomba makubwa hitilafu inapojitokeza.

# Sirari waomba bidhaa za nje zipunguzwe kodi

**Na Dinna Stephano,** TARIME

WANANCHI na wafanyabiashara wa Kata ya Sirari, wilayani Tarime mkoani Mara, wameiomba serikali kupunguza kodi kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kutoka Kenya ili kukomesha biashara ya magendo.

Wafanyabiashara hao wametaja bidhaa hizo kuwa ni pamoja na saruji, sukari na mafuta ya kula.

Wananchi hao wameiomba serikali kushusha kodi kwa bidhaa ya saruji inayotoka nchini Kenya ili iwe rafiki kwa wafanyabiashara ikizingatiwa kwamba Wilaya ya Tarime imepakana na nchi hiyo.

Wananchi hao walieleza hayo kwa Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, Mwita Waitara, alipokuwa katika ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Waitara ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), alisikiliza kero mbalimbali zinazowakabili.

Diwani wa Kata ya Sirari, Amos Sagara (CCM), alisema wananchi hawakwepi kulipa kodi, lakini kinachosababisha wapitishe bidhaa kwa njia za panya wanakwepa kodi kubwa kwa kuwa inawaumiza kibiashara.

"Wananchi hawakwepi kulipa kodi tatizo lipo serikalini wameweka kodi kubwa sana unapoingiza bidhaa za Kenya angalau saruji wangetoza hata Sh. 3,000 kwa kila mfuko. Wakikamatwa na bidhaa za Kenya wanapigwa kwa mipini ya jembe, pikipiki zimekamatwa wafanyabiashara wa bidhaa wanateseka, watu wanahitaji kupewa maelekezo, kodi za bidhaa na punguzo la malipo ya kodi kwa bidhaa zitokazo Kenya serikali ikifanya hivyo hakuna atakayekwepa kulipa kodi," alisema Sagara.

Chacha Mwita, mkazi wa eneo hilo, alisema Kata ya Sirari imepakana na Kenya na bidhaa za nchi hiyo zina bei nafuu ikilinganishwa na za Tanzania na kuwa kitendo cha kuzizuia ni kuwaumiza wananchi wa mipakani.

"Saruji ya Tanzania mfuko mmoja unauzwa Sh. 22,000, bado usafiri na wakati mwingine upatikanaji wake ni wa shida, mpakani Kenya saruji inauzwa kwa Sh. 12, 000 hadi 13, 000, ikiingia Tarime inauzwa Sh. 17,000 na upatikanaji wake ni rahisi," alisema Chacha.

Mbunge Waitara alisema kuwa saruji imekuwa ni tatizo kubwa kwa wananchi wilayani Tarime na kutaka suala hilo liangaliwe zaidi kwa kuwa linawaumiza wananchi na kuahidi kulifikisha mamlaka husika ili litatuliwe.

Wananchi hao pia waliomba kupo kwa mnada wa ng'ombe, huku wengine wakilalamikia vitendo vya uonevu vinavyotendwa na askari wa usalama barabarani.

Mbunge Waitara aliwasisitiza viongozi wakiwamo madiwani kufanya mikutano ya wananchi na kusikiliza kero zao pamoja na ushirikishwaji wa miradi ya maendeleo.

# Wakuu wa shule wasimamishwa kushindwa kusimamia ujenzi

**Na Thobias Mwanakatwe**

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amewasimamisha kazi wakuu wa shule wawili wa sekondari za Bahati Day na Muktuka katika Halmashauri ya Babati mjini kwa kushindwa kusimamia ujenzi wa mabweni ya shule hizo na kutumia gharama kubwa za ujenzi tofauti na mwongozo wa serikali.

Alichukua uamuzi huo baada ya kukuta kila shule imetumia zaidi ya Sh. milioni 80 na ujenzi umefikia hatua ya upauzi huku taarifa za gharama za shule hizo zikiwa zimefanana kwa kila kitu.

**Kila shule imetumia zaidi ya Sh. milioni 80 na ujenzi umefikia hatua ya upauzi huku taarifa za gharama za shule hizo zikiwa zimefanana kwa kila kitu.**

Kufuatia hali hiyo, Silinde aliagiza uchunguzi wa kina ufanyike kujua fedha hizo zimetumikaje na hatua kali za kisheria zichukuliwa kwa watu wote waliohusika katika matumizi mabaya ya fedha.

Pia alitangaza kuvunja kamati zote za ujenzi za shule hizo na kuagiza ziundwe upya na kuteuliwa makamu wakuu wa shule watakao simamia ujenzi huo mpaka kukamilika wakati uchunguzi ukiendelea.

Silinde alimwagiza Ofisa Elimu wa Sekondari Babati Mjini kuandika barua kwenda ofisi ya TAMISEMI ya kujieleza kwanini asichukuliwe hatua za kinidhamu kwa kushindwa kusimamia miradi hiyo huku mhandisi wa halmashauri hiyo akikutana na rungu hilo la kuandika barua ya kujieleza kwa kutoa ushauri ambao si sahihi wa matumizi ya bei ya juu ya ujenzi tofauti na maelekezo ya serikali.

Silinde pia, alitembelea Halmashauri ya Babati Vijijini kuangalia ujenzi wa mabweni mawili yaliyojengwa kwa Sh. milioni 74 kati ya Sh. milioni 160 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema hatua zilizochukuliwa ni kuunda kamati ya uchunguzi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kutokana na kutoridhika na gharama za ujenzi wa mabweni hayo mawili.



Mbunge wa Jimbo la Kiteto, mkoani Manyara, Edward Ole Lekaita (kushoto), akiwa na wananchi wa eneo hilo, wakielekea katika chanzo cha maji Kata ya Dongo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Mbunge ashauri leseni 201 za madini kufutwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MBUNGE wa Jimbo la Ludewa mkoani Njombe, Joseph Kamonga, ameshauri serikali kufuta leseni 201 za wamiliki wa vitalu vya madini wilayani Ludewa ambao hawafanyii kazi maeneo hayo.

Ushauri huo aliutoa mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa wa Njombe (RCC), baada ya kupata taarifa kutoka kwa Kaimu Ofisa Madini, Fredrick Jirenga, kuwa wilaya hiyo ina jumla ya leseni 201 za umiliki wa maeneo ya madini, lakini kati ya hizo zinazofanya kazi ni tano pekee.

"Naishukuru ofisi ya madini Mkoa wa Njombe kwa kuweka data hizi hadharani, zamani haikuwa hivi tumeambiwa Wilaya ya Ludewa zipo leseni za madini 201, lakini zinazofanya kazi ni tano pekee, nashauri leseni hizi zifutwe bila kujali mmiliki ni nani ili kutoa nafasi kwa wachimbaji wadogo wenye uwezo wa kuyafanyia kazi maeneo hayo," alisema Kamonga.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrea Tsere, alisema kuna maeneo yapo nje ya miradi ya Liganga na mchuchuma wilayani humo ambayo yalipaswa kumilikiwa na wachimbaji wadogo, lakini yamechukuliwa na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na kuwanyima fursa wachimbaji hao jambo ambalo linapaswa kutazamwa ili shirika hilo liwaachie na kutoa fursa kwa wachimbaji wadogo.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Marwa Rubirya, alisema serikali inaendelea kupitia mkataba wake na mwekezaji ambao ulikuwa unampa faida zaidi mwekezaji kwa asilimia 80, huku serikali ikibaki na asilimia 20 pekee na kwamba ofisi yake itawasilisha ombi kwa Rais John Magufuli la kuanza kuifanyia kazi miradi hiyo.

# NHIF kunufaisha wakulima 300 'Ushirika Afya'

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kupitia fao lake mahsusi kwa wakulima wa pamba linalojulikana kama 'Ushirika Afya' unatarajia kutoa huduma ya matibabu kwa wakulima 300 wa zao hilo kwa gharama ya Sh. 200 kwa siku ambazo ni sawa na 76,800 kwa mwaka.

Meneja wa NHIF mkoani hapa, Dk. Mohamedi Kilolile, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

"Niwaombe wakulima wa pamba wachangamkie fursa hii kwa kujiandikisha ili kupata huduma ya fao hili la 'Ushirika Afya' sababu maradhi hayapigi hodi. Sifa za kupata huduma hii ni sharti kwanza uwe mkulima wa pamba na pili uwe mwanachama wa AMCOS," alisema Kilolile.

Alisema gharama ya fao hilo kwa mkulima mmoja ni Sh. 76,800 kwa mwaka huduma ambayo imetajwa kuwa nafuu zaidi ambayo kwa mgawanyo wa malipo kwa mwaka ni sawa na mkulima kulipia Sh. 200 kwa siku.

Kilolile alisema kwa sasa huduma hiyo imeanza kutolewa kwa maeneo mengine na NHIF kwa kushirikiana na Benki ya Posta nchini (TPB), zimeungana ili kurahisisha utoaji wa fao hilo kwa utaratibu wa benki husika kumwazima huduma husika mkulima na kisha kurejesha malipo ya baada ya kuuza mazao yake.

"Mpaka sasa Mkoa wa Singida tumekwisha tembelea AMCOS 31 na kufanikiwa kuandikisha wanachama 300 wanaojishughulisha na kilimo cha pamba na zoezi bado linaendelea kabla ya mfuko kwa kushirikiana na TPB kuanza kuwanufaisha na fao hili," alisema.

Akizungumzia huduma nyingine zinazoendelea kutolewa mpaka sasa kwa Watanzania wote na zilizofanyiwa maboresho, Kilolile alisema mpaka sasa mfuko huo unatoa huduma ya vifurushi vya aina tatu vinavyoendana na ngazi ya uchumi wa kila mteja kumudu gharama yake kwa ubora stahiki.

Alivitaja vifurushi hivyo kuwa ni cha 'Najali' ambacho gharama yake kwa mtu mmoja ni Sh. 192,000 kwa mwaka, pia kifurushi kingine ni 'Wekeza' ambacho mtu mmoja ni Sh. 384,000 kwa mwaka na 'Timiza' kwa mwaka ni Sh. 516,000.

Pia alisema huduma ya vifurushi vyote hutolewa kwa mgawanyo wa makundi rika kati ya umri wa miaka 18-35, 36-59 na zaidi ya 60.

Vilevile, fursa nyingine ya vifurushi hivyo 'Najali' pamoja na kugharamia Bima ya Afya kwa mwaka mzima pia hutoa fursa ya mgonjwa kupatiwa huduma ya kulazwa wodini kwa siku 30, huku 'Wekeza' ikitoa siku 45 na 'Timiza' kikitoa siku 60 kwa huduma hiyo ndani ya mwaka.

"Chaguo ni lako. Niwasihi wanaSingida na Watanzania kwa jumla changamkieni huduma hizi kwa ustawi wa afya katika muktadha wa ujenzi imara wa taifa letu. Ugonjwa huwa haumwandai mtu...unaweza kuazima nauli ya kwenda mahali fulani na ukapewa, lakini huwezi kuazima fedha ya kwenda kwenye matibabu kwa sababu hujui matibabu hayo yatagharimu kiasi gani cha fedha," alisema Kilolile.

# Barabara ya Nyahua-Chaya kukamilika Machi 2021

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, amesema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa barabara ya Nyahua - Chaya (kilomita 85.4) inayojengwa kwa kiwango cha lami na mkandarasi China Henan International (CHICO).

Alisema kukamilika kwa barabara hiyo ambayo ni sehemu ya barabara kuu ya Tabora - Nyahua - Chaya - Itigi - Manyoni, yenye jumla ya urefu wa kilometa 259 kutapunguza urefu wa safari kwa kilometa 191 kwa magari yanayopitia barabara ya Tabora - Nzega - Singida hadi Manyoni na kuleta tija kwa wasafiri na wasafirishaji wa mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi.

**Hakikisheni sehemu ya kilomita sita zilizobaki kuwekwa lami zinakamilika kabla ya mwezi Machi ili kuwezesha wananchi kunufaika na barabara hii.**

"Hakikisheni sehemu ya kilomita sita zilizobaki kuwekwa lami zinakamilika kabla ya mwezi Machi ili kuwezesha wananchi kunufaika na barabara hii," alisema Kasekenya.

Aliwataka wakazi wa Mkoa wa Tabora kuilinda miundombinu ya barabara, madaraja na taa za barabarani ili zidumu kama ilivyokusudiwa.

Naye Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROAD), Mkoa wa Tabora, Damian Ndabalinze, amemhakikishia Naibu Waziri Kasekenya kuwa mkoa huo umejipanga kulinda barabara zake na kuziwekea taa sehemu nyingi ili kuongeza usalama na kupendezesha mji huo.

Zaidi ya Sh. bilioni 117 zimetumika katika ujenzi wa barabara ya Nyahua - Chaya ambayo imehusisha ujenzi wa madaraja makubwa mawili ya Nyahua na Kizengi, mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, mwaka huu.

Kasekenya yupo mkoani Tabora kwa ziara ya siku mbili ya kukagua miundombinu inayoendelea kutekelezwa mkoani humo.




Meneja Mwandamizi Ukusanyaji wa Amana Benki ya CRDB, Abel Lasway (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kutangaza washindi wa kampeni ya benki hiyo, iliyotambulika kama "Tumekusoti Ada" iliyoendeshwa katika kipindi cha Desemba kwa wateja waliofungua akaunti ya watoto (Junior Jumbo) na kuweka akiba. Jumla ya wateja 20 wameibuka washindi. Wengine pichani ni Meneja Mauzo wa Benki ya CRDB, Elikira Nkya (kulia) na Meneja Uhusiano wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Bupe Makibi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tabata yajipangia mikakati kuboresha barabara

**Na Maulid Mmbaga**

MWENYEKITI wa CCM Kata ya Tabata, Sudi Khasim, amebainisha mipango mkakati ya kimaendeleo wanayo tarajia kuitekeleza kwa mwaka 2021 ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara.

Akizungumza na wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika kikao cha halmashauri kuu ya kata kilichofanyika jana, aliwasisitiza viongozi kufanya kazi kwa bidii ili kuendelea kukipa uhai chama hicho.

Alisema wananchi waliwachagua viongozi wa chama hicho, ili wakawatatulie kero zinazowakabili kwa kipindi kirefu na kwamba ni wajibu wao kufanya kazi kwa bidii ili kuendana na kasi ya serikali.

"Bila kufanya kazi kwa bidii itakuwa ngumu kushinda uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, tushughulikie changamoto za wananchi tuzunguke katika maeneo yetu ili iwe rahisi kutambua yanayowakabili wananchi na tuyatatue kwa wakati," alisema.

Alisema kumekuwa na malalamiko ya mipaka kwa baadhi ya wakazi wa eneo hilo na kuahidi kwa kushirikiana na viongozi wenzake watalifikisha mahali husika ili yaweze kutatuliwa.

Katibu wa CCM wa kata hiyo, Haruna Alphonce, alisema tangu waingie madarakani wamekuwa wakitekeleza matakwa ya katiba ya kufanya vikao vya halmashauri kuu ya kata vikiwa na dhumuni la kubainisha na kuweka mipango mikakati ya kutatua kero zinazowakabili wananchi.

Alisema mikakati yao ndani ya mwaka 2021 ni pamoja na kuimarisha miundombinu ndani ya kata hiyo ikiwa ni pamoja na kutengeneza mifereji ya kupitisha maji ya mvua ambayo yanasababisha mafuriko kutokana na kukosa mikondo maalumu.

"Jambo lingine ni suala la taka ambalo limekua miongoni mwa changamoto kubwa ndani ya kata yetu tumeweka mkakati wa kuongeza gari litakalotumika kuzoa taka hizo na kuyaacha maeneo yetu yakiwa safi," alisema.

Aliwataka wakazi wa kata hiyo kujitahidi kuzingatia usafi wa mazingira kwa kutotupa taka ovyo kuepuka magonjwa ya milipuko na kuhatarisha afya zao.

## Ngawaiya atoa salamu za mwaka mpya kwa vijana

**Na Sabato Kasika**

VIJANA wametakiwa kuchangamkia fursa za kilimo vijijini badala ya kukimbilia mijini kutafuta maisha.

Wito ulitolewa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, wakati akitoa salamu za mwaka mpya za taasisi hiyo.

Alisema mwaka 2021 unatakiwa uwe ni mwanzo wa vijana kuachana na mawazo ya kukimbilia mijini kufanya biashara ndogo na kugeukia kilimo ambacho kina fursa ya kuwaletea maendeleo.

"Ukifuatilia utagundua kuwa kwa sasa serikali imeamua kuwainua wakulima ikiwa ni pamoja na kutaifisha mashamba makubwa yaliyokuwa hayatumiki na kuwagawia wakulima," alisema Ngawaiya.

Alisema, hatua hiyo inaonyesha ni jinsi gani serikali inataka kuwainua wakulima na kuwataka kuachana na biashara ya kimachinga na kufuata utajiri uliopo kwenye kilimo ambao upo nje.

"Kwa mfano, wakati wa corona, baadhi ya nchi zinazotuzunguka zimefungia wananchi wao ndani, hivyo ni wazi zitakuwa na mahitaji makubwa ya chakula, sasa hii ni fursa kwetu kulima kwa wingi ili baadaye tuwauzie," alisema.

Aliongeza kuwa wakati huu ambao Tanzania inaelekea kuwa ya viwanda, kuna haja ya kujikita kwenye kilimo zaidi kwa vile ndiko kunakotoka malighafi za viwandani.

"Sisi watu wa taasisi ya utawala bora, tuna wajibu wa kuwakumbusha Watanzania na kuelekeza kwenye fursa mbalimbali zitakazowasaidia kujiletea maendeleo na tunaona kilimo ni mojawapo ya fursa," alisema.

Alifafanua kuwa Tanzania ina eneo kubwa linalofaa kwa kilimo, lakini linalotumika ni dogo, kutokana na watu wengi kutotambua fursa hiyo na kujikita kwenye umachinga.


"CEGODETA inaamini kwamba, vijana wenye nguvu ya kufanya kazi hawawezi kushindwa kulima mazao ya chakula na biashara, hivyo mwaka 2021 uwe wa kubadili mawazo yao ili wachangamkie fursa zilipo kwenye kilimo," alisema.

Aliwataka vijana kutokata tamaa na kuendelea kujiajiri katika fursa walizonazo zikiwamo ardhi ya kilimo kwa kutumia nguvu walizobarikiwa kwa vile serikali imeshaweka mazingira wezeshi katika sekta hiyo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 12, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 14

Maabara zinavyogeuzwa madarasa kuokoa jahazi


Ukurasa 13

JPM uhai mpya fikra Karume na Nyerere

TEKNOLOJIA
NA GAUDENSIA MNGUMI

## MAPINDUZI DAY

# NI JUKWAA LA KARUME

■ SUZA kuanzisha 'kiti' kuzienzi fikra na kazi

NI miaka 57 baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964, yaliyokata minyororo na kuwaweka huru Waafrika, waliovuja jasho bila ujira kuujenga uchumi wa Zanzibar kwa manufaa ya wachache. Hao walikuwa wakwezi wa minazi na karafuu, wavuvi, vibarua mashambani, watumwa na watwana ambao walikandamizwa na kuumizwa na utawala wa kisultani.

Leo ndiyo siku ambayo historia inatuambia mwanasiasa Sheik Abeid Aman Karume, alizipindua meza kibabe za ikulu ya sultani na kuuangusha utawala wa Sultan Jamshid bin-Abdullah aliyezaliwa mwaka 1929, na kuanza kuiongoza Zanzibar 1963 hadi 1964, aliangushwa na wapigania uhuru, wazalendo wana Afro Shiraz wakiongozwa na Karume.

Ni karibu miongo sita (miaka 60) sasa, taifa linaendelea kuyaenzi Mapinduzi ya Zanzibari na kazi kubwa iliyofanywa na Karume kuunda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Baraza la Mapinduzi.

Kwa kuangalia uhai wa kiongozi huyu katika siasa, ni wazi kuwa miaka nane aliyoiongoza Zanzibar kuanzia 1964 hadi 1972 ni muda mfupi, lakini anatajwa kufanya mambo makubwa. Yataonekanaje, taifa na Wazanzibari wanayaenzi vipi mapinduzi na kazi za Karume ili zisisahaulike? Ni nini kinafanyika kuvifanya vizazi vya sasa na vijavyo kuuenzi mchango wake kwenye ukombozi?



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Zakia Abubakar, akimkabidhi vitendea kazi Mkuu wa Chuo na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, baada ya kusimikwa rasmi kuwa mkuu mpya wa chuo hicho hivi karibuni. Taasisi hiyo ndiyo inayoratibu uanzishwaji wa Kiti cha Karume. **PICHA: PRO SUZA**

Swali hili linajibiwa na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), katika mahojiano na Mhadhiri Dk. Sarah Seme, anayeieleza Nipashe kuwa Karume hatasahaulika kwenye fikra za Watanzania na kama ilivyo kwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kupitia Kigoda cha Taaluma cha Mwalimu Nyerere, juhudi za kuhifadhi na kuenzi historia ya Zanzibar ya Mapinduzi ya mwaka 1964 na mambo ya kutukuka ya Rais wa kwanza wa Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume yanafanyika.

Anasema kazi hizo zina historia ndefu ndani ya madhumuni ya uanzishwaji wa SUZA, ndiyo maana kitengo cha historia kwa kushirikiana na menejimenti, wadau wa ndani na nje ya Zanzibar wamefanya shughuli mbalimbali za kufanikisha juhudi hizi hatua kwa hatua, mojawapo ni zile zinazohusisha au kugusa moja kwa moja kumuenzi Karume kwa kuanzisha Kigoda cha Sheikh Abeid Amani Karume na mchakato wa kuanzishwa kwake kunafikia hatua za ukamilifu.

"Hivyo nisema bila shaka si muda mrefu kigoda kitaanza kufanyakazi rasmi," anasema Dk. Sarah wa Kitengo cha Historia SUZA.

Analiambia gazeti hili kuwa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, kinaanzisha Kiti cha Utafiti (University Research Chair) ambacho kitakuwa cha kwanza katika historia ya SUZA, ambacho madhumuni yake makuu ni kumuenzi Rais wa kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Sheikh Abeid Amani Karume.

Anaongeza kuwa Kiti cha Utafiti cha SUZA kinaazimia kuyaenzi mawazo na fikra za Karume ambaye amekuwa ni miongoni mwa wanaharakati na wanamapinduzi wakubwa waliopambana kwa nguvu zote kuhakikisha Zanzibar na Afrika zinakuwa huru ili kujiletea maendeleo kiuchumi na katika nyanja nyingine za maisha.

Kama kilivyo kwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kitaitwa Kiti cha Utafiti cha Sheikh Abeid Amani Karume katika Ukombozi na Maendeleo ya Afrika (SUZA) 'Sheikh Abeid Amani Karume Professorial Chair in Liberation and Development of Africa.'

**MALENGO MAKUU**

Kiti cha Utafiti cha Karume lengo lake kuu ni pamoja na kuhifadhi, kuenzi na kuendeleza mawazo na fikra za Sheikh Abeid Amani Karume katika kuleta ukombozi na maendeleo ya Zanzibar, Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla, kupitia utafiti na mijadala mbalimbali ya kisomi kutoka kwa wadau na wataalamu wa utafiti wa kada mbalimbali.

"Ni ili kukabiliana na changamoto mbalimbali katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kisayansi na kifikra na kufanya SUZA kuendeleza azma yake ya kuwa kichocheo cha mabadiliko ya jamii." Anaongeza mhadhiri huyo.

Ili kufanikisha malengo hayo kutakuwa na kuhifadhi, kuibua na kueneza mawazo na fikra za Sheikh Abeid Amani Karume kupitia utafiti, mijadala, makongamano, mikutano pamoja na machapisho mbalimbali kuzungumzia kazi zake.

Kuandaa na kutekeleza mipango na kazi za kila siku za kiti ikiwamo programu za kuelimisha, kushajihisha (kuongeza uelewa) na kuenzi kwa vitendo fikra na falsafa za Karume kupitia shuleni, vyuoni na ndani ya jamii.

Dokta Sarah anataja kuwashajihisha wananchi kuhusu fikra za Karume kupitia mikutano, mijadala,

INAENDELEA UK.12

## MAPINDUZI DAY

# NI JUKWAA LA KARUME

INATOKA UK.11

machapisho na mihadhara ya wazi.

Pia kukusanya makala na kazi mbalimbali zilizoandikwa kuhusu kiongozi huyo wa kwanza wa Zanzibari.

Anasema kingine ni kukifanya Kiti cha Utafiti SUZA kuwa ni mahali pa majadiliano na mijadala ya kupitia shughuli mbalimbali kama makongamano, mikutano na machapisho mbalimbali yahusuyo maendeleo ya mtu binafsi na taifa katika kuenzi falsafa za Karume.

Anataja jingine kuwa ni kukuza uwezo wa vijana na wasomi wanaochipukia kwa kuwashirikisha katika utafiti, makongamano, mikutano na mijadala mbalimbali ya kiti na kuwapa mafunzo yanayoendana na malengo ya kiti cha Karume na kuwasaidia kupata fedha na mikopo ya masomo na utafiti, kwa mujibu wa maelezo yake.



Wasomi wa Chuo cha SUZA wakiwamo timu inayoandaa Kiti cha Karume pamoja na Mkuu wa Chuo, Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: SUZA**

### KUVUKA MIPAKA

Dokta Sarah anasema kiti kitaendeleza ushirikiano ndani na nje ya Afrika kuendeleza yaliyoanzishwa na Sheikh Abeid Amani Karume kabla na baada ya mapinduzi katika harakati za kupigania ukombozi na maendeleo ya Zanzibar na Afrika. Kitaanzisha uhusiano mpya na wadau wakiwamo watu binafsi, taasisi za kiserikali, za kiraia za ndani na nje ya nchi ili kuendeleza harakati za kuleta maendeleo ya Zanzibar, Tanzania na Afrika.

Anapowalinganisha Nyerere na Karume, kwenye mrengo wa kazi za kitaaluma, Dk. Sarah, anakiri kuwa Karume si mwanataaluma kama alivyokuwa Nyerere hivyo ni mara chache kukuta machapisho yake na kazi zake nyingi kama ilivyo kwa Baba wa Taifa.

"Kazi za mwanamapinduzi huyu hazikuwa katika mwelekeo wa kitaaluma (vitabu, majarida), lakini kiti cha utafiti cha Karume lengo lake ni pamoja na kupata fikra na mawazo yake na kuzienzi kwa vitendo na wadau mbalimbali wakiwamo wanataaluma watahusika.

Hivyo kidoga chake kinakusanya, kuhifadhi na kusambaza matendo na kazi za Sheikh Karume zilizo kwenye maandishi, kumbukumbu za wadau alioshirikiana nao au kufaidika na kazi zake ili kuzipa muonekano wa kitaaluma unaosomeka na kuhifadhika," anaeleza.

"Kiti cha Utafiti cha Karume kinalenga kukusanya na kuhifadhi kazi zake mbalimbali zikiwamo kumbukumbu za hotuba, mihadhara, mikutano, machapisho, picha za matukio ya utekelezaji wa harakati za ukombozi na maendeleo, kama vile ya utaifishaji na ugawaji wa ardhi, ujenzi wa nyumba kwa maskini, kushiriki kilimo mfano cha karafuu na kuziweka katika maktaba maalum itakayoanzishwa na kigoda hiki. Kazi hizo kwa mujibu wa mhadhiri huyo zitasambazwa kupitia 'forum' mbalimbali za jamii.

### MAMBO ENDELEVU

Anasema ili kulifanya lengo la kiti kuwa endelevu SUZA na vyuo vikuu vingine vitaimarisha masomo ya historia, 'heritage', akiolojia (elimu ya mambo ya kale) na taaluma za maendeleo 'development studies' na kuanzisha masomo yanayoendana na Kiti cha Utafiti cha Karume katika ngazi zote za elimu ili kuwajengea vizazi vya sasa na vijavyo msingi na historia sahihi ya ukombozi na maendeleo ya nchi, Afrika na dunia kama ambavyo Sheikh Abeid Karume aliamini kuwa elimu ni msingi wa maendeleo kwa kuleta elimu bila malipo.

Mhadhiri huyu na mmoja wa wanataaluma washiriki wa kuanzisha Kidoga cha Karume anataja kukusanya kazi zilizoandikwa kuhusu kiongozi huyo na kuendeleza tafiti zaidi kwa wanataalum ili waendelee kuandika na kuzisambaza zaidi kwa manufaa ya taifa lakini pia kuenzi mchango mkuwa wa kiongozi huyo.

"Kwa mfano kwa kushirikiana na watafiti wa "Southern Africa Liberation Sturggles kupitia Umoja wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika ( SADC) Hashim Mbita Project tumeandika mchango wa Karume katika harakati za ukombozi wa Afrika na watu wake katika Kitabu cha Tanzania and Liberation Struggles of Southern Africa, 1961-1994 kilichochapishwa mwaka 2014 na kampuni ya Mkuki na Nyota. Ndani yake kinaonyesha mchango mkubwa wa Zanzibar chini ya Sheikh Abeid Amani Karume kwenye harakati za ukombozi," anasema Sarah.

Anakumbusha kuwa kwa andiko hilo, watu mbalimbali na wadau walitoa uzoefu wao juu ya mchango wa Zanzibar katika ukombozi wa Afrika, kwa hiyo hizo ni baadhi ya kazi kati ya majukumu ya Kidogo cha Karume ambazo zitaenzi mchango wake uliotukuka hasa kwa jamii ya wanyonge.

### ULINGANIFU WA 'VIGODA'

Mhadhiri wa Historia katika Shule Kuu ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (DUCE) Samwel Mhajida, anasisitiza kuwa Kigoda cha Karume ni muhimu ili kuenzi kazi zake.

Anasema Karume ni zao la siasa waliokandamizwa, kuonewa na kunyanyaswa na utumwa na ukoloni wa kisultani. "Ni tunda la siasa za vitendo na uhalisia, kutoka jamii ya waliochoshwa na utawala kandamizi wa kisultani. Ni mwanasiasa anayeibuka kutoka kundi la wakandamizwaji, wanaopambana na uonevu na dhuluma." Anasema.

Historia ya Zanzibar iliyoanza mwaka 1964 inayohusisha kutetea wanyonge na watu ambao hawakuwa na nafasi kama ambao hawakuwa na mtetezi imeandikwa juu ya Karume hivyo ni lazima kuihifadhi.

### MAMBO YANAYOISHI

Anasema Kigoda hicho ni muhimu kwani kinaakisi yale Karume aliyoyalenga kama kuwawezesha Wazanzibari waliokuwa watumwa wa ukoloni wa kisultani kupata haki na uhuru.

"Amefanya mambo yanayoishi hadi leo kwa mfano kuanza sera ya kutaifisha na kugawa ardhi kwa Wazalendo, kuwapa heka tatu za ardhi kwa kila mmoja ili alime na kuinua uchumi wake, familia na taifa. Si hilo tu aliwapa makazi bora Wazanzibari alijenga nyumba za kisasa za ghorofa ziko Michenzani Unguja na Micheweni Pemba na pia kuna nyumba nyingine sehemu nyingi ili wapate makazi wale ambao hawakuwa nayo," anakumbusha Mhajida.

Baada ya mapinduzi, anaanza kuwapa watoto wa wafanyabiashara, wachuuzi, wakwezi, wakulima na makuli elimu bora, afya, makazi na njia bora zaidi ya mawasiliano kwa kuwapa kituo cha televisheni ya taifa cha rangi, ikiwa ndiyo ya kwanza barani Afrika Kusini ya Jangwa Sahara, si jambo la kusahaulika.

Mhadhiri huyu anaunga mkono juhudi za SUZA, akisema Karume amefanya mambo makubwa akishirikiana na watu wa hali ya chini, viongozi wenzake akiwamo Nyerere na wakuu wengine wa Afrika kuleta uhuru wa bara hili, kwa hiyo ni vyema SUZA kufanya utafiti na kuibua mengi muhimu yanayokikamilisha Kidoga cha Karume.

"Ni vyema kianzishwe ili fikira zake ziendelee kubaki na kudumu kwenye vizazi vya Watanzania wa sasa na wajao. Mwanzo wa kuenzi viongozi wachapa kazi na kutambua juhudi za kiongozi huyo aliyeongoza Zanzibar kwa miaka nane kabla ya kuua 1972."

### KIGODA CHA NYERERE

Anapoulizwa pengine Watanzania wanaweza kuuliza kwanini kumekuwa na Kigoda cha Mwalimu kwa miaka mingi lakini hakikuwapo cha Karume? Anajibu:

"Nisema kuwa Kigoda cha Mwalimu kiliwahi kuanzishwa au kuwapo mapema kwa sababu ya falsafa zake kukubalika, kuheshimiwa na kutambuliwa zaidi kwenye taaluma kwa sababu ameshiriki sana kwenye masuala ya kitaaluma."

Mwalimu Nyerere amechangia maendeleo ya taaluma nchini, amekuwa karibu na wanataaluma na kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, amekuwa Mkuu wa Chuo kwa miaka mingi.

Mwalimu Nyerere amekuwa mlezi wa Chama cha Wanahistoria wa Tanzania ambao ni wanataaluma. Amekuwa akishirikiana na wasomi, ni kama ilikuwa sehemu yake, kwenye mijadala ya kitaaluma alikuwapo. Mara nyingi akiwa msemaji mkuu na wakati mwingine ni mshiriki wa mijadala, ni mchangiaji mkubwa wa maendeleo ya elimu kwenye taasisi za elimu ya juu na hotuba zake zenye kusisimua zimekuwa sehemu ya nukuu zinazotumiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kwingineko. Mathalani, nukuu iliyoko katika utambulisho wa Maktaba Mlima inakariri sehemu ya hotuba zake, inayowaasa wasomi kuthamini wajibu wao kwa wananchi ambao wanategemea elimu yao ilite tija kwa mamia ambao hawajasoma wanaoishi vijijini."

Anasema Mwalimu Nyerere kwenye uwanja wa taaluma anaishi na ni bingwa wa tafakari zenye kusisimua na kuendeleza fikra tunduizi (critical thinking), kila kazi zake zinaposomwa ama kusikilizwa.

Anasema yote haya yamewezesha kuanzishwa kwa Kigoda cha Mwalimu ambacho kipo kwenye nyanya za taaluma.

### DHANA YA KIGODA

Mhajida anapoulizwa Kigoda maana yake ni nini hasa kinapohusishwa na viongozi hao waasisi na wanasiasa? Anasema, kinamaanisha kuwa ni eneo la kukaa au 'palavar' sehemu ambayo wazee wa zamani wa Afrika walikutana kujadili jambo kwa kina na kupata ufumbuzi.

"Ni kama sehemu ambayo wazee walikutana na kuweka sawa masuala ya msingi na ya maendeleo kwenye jamii zao. Hakukuwa na utaratibu rasmi wa kuwa na mwenyekiti, katibu na wengineo lakini kazi ilifanyika na maamuzi yalifikiwa, ndipo dhana inapoanzia.

"Leo ni sehemu ya watu kujadili Utanzania wetu, uchumi na utaratibu wa kuenzi urithi (legacy) wa Nyerere ili kuendelea kumkumbuka."

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

MAPINDUZI DAY

# JPM uhai mpya fikra Karume na Nyerere

■ Wanyonge kwanza, elimu, mikopo kwa wote



AGOSTI 4, 1905 ndiyo siku aliyozaliwa Sheikh Abeid Amani, Karume (pichani) aliyeongoza mapinduzi ya Januari 12, 1964 yaliyomng'oa Sultan Jamshid bin-Abdullah, lakini kiongozi huyo akafariki dunia Aprili 7, 1972, baada ya miaka minane ya kuwaongoza Wazanzibari.

Akiwa ni mwanasiasa aliyetokea kwenye viunga vya watu wa hali ya chini, Karume alikuwa kiongozi mtetezi wa wanyonge ambaye aliyatazama mateso ya watumwa, watwana (watumwa wa kiume), wakwezi wa minazi na karafuu, wavuvi wa samaki na pweza, wakulima, makuli wafanyao kazi bandarini kwa ujira kiduchu licha ya kusota chini ya jua kali na kuvuja jasho jingi, akaamua kuwapa zawadi ya ukombozi kupitia mapinduzi yaliyounda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ilikuwa si kazi rahisi, kumpindua mkoloni ikulu na kuchukua nchi, ndiyo maana wapo wanaomuona Karume kuwa ana hadhi ya kipekee barani Afrika, kufanya mapinduzi ya kishupavu.

Ni mtetezi wa wanyonge aliyehatarisha maisha yake kwa kuwafanya mapinduzi ya kuwaangusha wakoloni na kwa muda mfupi kuwaunganisha waliokandamizwa, kuwasikiliza na kuwaandalia mipango ya kuwaendeleza kwa kila hatua baada ya kuwarejeshea uhuru wao.

**FIKRA ZAKE ZINAZOISHI**

Mapinduzi ya 1964 visiwani Zanzibar yaliyofanikishwa na Karume na Uhuru wa Tanzania mwaka 1961 uliopatikana kwa juhudi za Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na viongozi wengine akiwamo Rashid Kawawa, ukilinganishwa awamu ya sasa wa Rais John Magufuli, unaendelea kuakisi fikra za kimapinduzi za waasisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wazanzibari na Watanzania wanamuona Karume kama shujaa, akitetea maskini wa hali ya chini, akiwainua waliodhulumiwa na kukandamizwa, kuonewa na kuteswa, ndiyo aliowapigania hata kufanya mapinduzi. Fikra za kupigania wanyonge na uzalendo zinaonekana leo kwa Rais John Magufuli, ambaye anaanza upya kusimamia rasilimali za taifa ili ziwanufaishe wananchi huku serikali ikigharamia elimu kwa watoto wote kama walivyofanya waasisi.

Anampa kila Mtanzania umeme kupitia mradi wa nishati vijijini (REA), serikali yake inachambua na kupitia upya mikataba ya madini ni miongoni mwa mambo ambayo fikra za Karume za kuwapa Watanzania maisha bora zinaendelea kuonekana ndani ya Magufuli.

Tangu awali Rais Magufuli analinganishwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere na kuonekana kuwa ndiyo mfano wake halisi, kwa kuibua mambo mengi ambayo Nyerere ameyafanya na anayaendeleza pamoja na fikra zake kwa ujasiri mkubwa wa kimapinduzi, unaomtofautisha na viongozi wengine wa Afrika, anasema Mhadhiri wa Historia wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) , Dk. Sarah Seme .

"Sisi sote tunaweza kuwa mashahidi wa hayo kama hata na ninyi mlivyoona. Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume wanafanana katika fikra hizi za kutetea wanyonye, kupambana na umaskini, kurudisha rasilimali na njia kuuza za uchumi kwa wakandamizwaji wa wanyonye na kufanya juhudi za makusudi kuwainua," anaeleza Mhadhiri Sarah.

Anasema kwa nyakati tofauti, juhudi hizi zilitiwa nguvu na siasa za ujamaa na kujitegemea ambazo zilipambana na unyonyaji na ukandamizaji wa kibepari na kibeberu. Kwa muktadha huo, Rais Magufuli anafanana na viongozi waasisi Nyerere na Karume, katika kuondoa dhuluma hasa uporaji wa mali ya umma kunufaisha wachache, kupitia rushwa, ufisadi, ubadhirifu na matumizi mabaya ya ofisi za umma.

Anapambana na ufisadi kwa juhudi kubwa kwa kuwa umedidimiza wanyonge, kutokuwajibika akiamsha upya maadili na uwajibika kwenye utumishi wa umma na kupambana na umaskini kwa kuwekeza kwenye miradi inayoleta na itakayokuwa na tija kama miundombinu, viwanda ili kuleta ajira kwa kujiajiri au kuajiriwa, anadokeza Dk. Sarah.

"Rais Magufuli anasisitiza umuhimu wa elimu, serikali inagharamia elimu na pia anaahidi kujenga sekondari za vipaji maalumu kila mkoa ni kwa sababu ndiyo mkombozi kama alivyoanza Nyerere na Karume. Rais anaendeleza fikra hizi za kimapinduzi kwa ujasiri, pasipo hofu kama ambavyo waasisi walivyofanya kwa ujasiri." Anaongeza.

"Kwa nyakati hizi za sasa za utandawazi Rais ametekeleza fikra za waasisi kwa ubunifu mkubwa, ili kuendana na wakati na tunaona amefanikiwa kwa asilimia kubwa. Katika nyakati za Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume, walisimama kwa ujasiri mkubwa kuondoa ukoloni na usultani, nyakati hizi Rais Magufuli anasimama kwa ujasiri mkubwa kupambana na mafisadi, wala rushwa, ukoloni mamboleo ili kuinua taifa na watu wake kutoka kwenye umaskini na kufikia uchumi wa kati." Anasema Dk. Sarah.

> "Rais Magufuli anasisitiza umuhimu wa elimu, serikali inagharamia elimu na pia anaahidi kujenga sekondari za vipaji maalumu kila mkoa ni kwa sababu ndiyo mkombozi kama...

Anakumbusha kuwa mwanamapinduzi Karume aliamini elimu ndiyo msingi wa maendeleo akaleta elimu bila malipo, vivyo hivyo Rais Magufuli anatekeleza fikra hizo kwa wanafunzi kusajiliwa, kusoma kuanzia elimu ya awali hadi sekondari bila wazazi na walezi kudaiwa ada na anaendelea mbele zaidi kufanya elimu ipatikane kwa viwango vya juu vya elimu kwa kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wengi zaidi kila mwaka mpya wa elimu.

ELIMU
**NA SABATO KASIKA**

# Maabara zinavyogeuzwa madarasa kuokoa jahazi

## Hakuna kusubiri awamu ya 2



Moja ya madarasa ya Shule ya Sekondari ya Seka, ambayo inatarajiwa kuanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

WAKATI shule zimefunguliwa kuanza mwaka mpya wa masomo jana, wanafunzi 155 wa kidato cha kwanza katika Halmashauri ya Musoma mkoani Mara, waliokuwa wasubiri kukamilika ujenzi wa madarasa, wako madarasani wakifurahia masomo ndani ya vyumba vya maabara.

Kwa nini imekuwa hivyo? Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, anasema, hakuna haja ya kuwa na maabara tupu, wakati ni darasa linaloweza kutumiwa na watoto badala ya kubakia nyumbani wakisubiri awamu ya pili, jambo linaloweza kukwamisha mipango ya kishule.

"Lengo ni kutaka wasiwapo wanafunzi watakaokaa nyumbani kusubiri awamu ya pili, tunataka wote waanze masomo kwa pamoja." Anasema na kuongeza kuwa watasomea kwenye maabara wakisubiri ujenzi wa madarasa kukamilika.

"Kwa pamoja tumefikia hatua hiyo kwa kuwa kuna umuhimu wa wanafunzi kuanza masomo kwa pamoja badala ya kuwaacha wapishane huku wote wakiwa ni wa kidato kimoja," anasema Dk. Anney katika mahojiano na Nipashe.

Wilaya ya Musoma ina halmashauri mbili ikiwamo manispaa na kwamba kwa upande wa Halmashauri ya Musoma yenye Jimbo la Musoma Vijijini kuna sekondari za kata 20.

"Vilevile kuna tano zinazoendelea kujengwa ili zianze kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka huu zikiwamo za Seka iliyopo Kata ya Nyamrandirira na Kigera kwa ajili ya wakazi wa kata ya Nyakatende," anaasema.

> "Kazi hiyo si kwa shule za sekondari tu bali za msingi na shikizi (awali), wamejitolea nguvukazi na fedha pia, lengo likiwa ni kuhakikisha kila shule inakuwa na miundombinu inayohitajika," anasema na kuongeza kuwa anaamini ujenzi wa madarasa utakamilika hivyo wanafunzi wote 4,089 watakapata madarasa na kusoma bila usumbufu.

Mkuu huyo wilaya anazitaja nyingine kuwa ni Nyasaungu iliyoko Ifulifu, Bukwaya ya Kata ya Nyegina na Ifulifu na kwamba ujenzi wake unakwenda kwa kasi.

**IDADI YA WALIOCHAGULIWA**

Jumla ya wanafunzi 4,089 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, katika sekondari za Halmashauri ya Musoma, lakini 155 kati yao walitakiwa kusubiri awamu ya pili ya kuanza masomo, kwa mujibu wa maelezo yake.

"Lakini tumetafakari na kuona hakuna mwanafunzi kubaki nyumbani, badala yake wasome katika majengo ya mabara kwa muda wa wiki mbili kisha waende kwenye madarasa yanayotarajiwa kukamilika wakati huko kusubiri nyumbani," anasema.

Wananchi kwa kushirikiana na serikali, wamefanya kazi kubwa hasa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa maktaba, maabara, nyumba za walimu, madarasa na vyoo, anasema mkuu wa wilaya.

"Kazi hiyo si kwa shule za sekondari tu bali za msingi na shikizi (awali), wamejitolea nguvukazi na fedha pia, lengo likiwa ni kuhakikisha kila shule inakuwa na miundombinu inayohitajika," anasema na kuongeza kuwa anaamini ujenzi wa madarasa utakamilika hivyo wanafunzi wote 4,089 watakapata madarasa na kusoma bila usumbufu.

**JEKI YA MFUKO WA JIMBO**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma, Charles Magoma anasema, Sh. milioni 52.43 za Mfuko wa Jimbo zimetumika kukamilisha ujenzi wa madarasa katika sekondari mbalimbali.

"Halmashauri yetu inayotunza fedha za mfuko huo inafanya manunuzi ya vifaa vya ujenzi baada ya kupata maelekezo kutoka kwenye Kamati ya Mfuko wa Jimbo chini ya Mwenyekiti ambaye ni mbunge Profesa Sospeter Muhongo," anasema Magoma.

Anafafanua kuwa Mkuu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Musoma, John Kayombo, wamefanya juhudu kubwa ya kusimamia ujenzi wa madarasa hayo.

Kuhusu mgawo wa fedha hizo anasema kilichofanyika ni pamoja na ununuzi wa mabati 1,134 na mifuko 1,020 ya saruji vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 52.18 ili kukamilisha miundombinu ya shule mpya ili zifunguliwe mwaka huu.

Mwenyekiti huyo anasema, sekondari za Seka na Kigera, kila moja ilipata mabati 216 na mifuko 200 ya saruji, huku Nyasaungu ikiwa na mgawo wa mabati 54 na mifuko 80 ya saruji.

"Hizo ni sekondari mpya, lakini mgawo wa vifaa umekwenda pia kwa zile zilizofunguliwa mwaka jana ikiwamo Dan Mapigano Memorial na Busambara ambazo zote kila imepata mabati 216 na mifuko 180 ya saruji," anasema.

Aidha, anasema shule shikizi ya Mwikoko iliopo kitongoji cha Mwikoko, Kijiji cha Chitare, Kata ya Makojo, imepata mabati 108 na mifuko 10 ya saruji, wakati ile ya Nyasaenge ya Kijiji cha Kataryo, Kata ya Tegeruka ikipata mabati 108 na mifuko 100 ya saruji.

**HATUA ZILIPOFIKIA**

Magoma anasema, shughuli zote za ujenzi wa miundombinu ya shule zimekuwa zikifanywa na wananchi, serikali, mbunge na wadau wengine wa elimu zikiwamo taasisi za fedha.

Anasema, kwa sasa kuna shule shikizi 12 na kwamba ujenzi na upanuzi wa shule hizo unaendelea, huku baadhi yake zikiwa tayari zimeanza kutoa elimu ya awali kwa watoto wa chini ya miaka sita.

"Halmashauri yetu ina shule 111 za msingi na sasa ujenzi wa madarasa mapya katika shule hizo unaendelea huku madarasa 380 yakiwa tayari yamejengwa kwenye shule hizo ndani ya miaka mitano kuanzia 2016 hadi 2020," anasema.

Magoma anasema, madarasa 120 yamejengwa kwenye sekondari 20 ndani ya miaka hiyo mitano na kuchangia sekonadari sekondari za Dan Mapigano Memorial na Busambara kufunguliwa mwaka jana.

Anasema jitihada hizo zinafanikishwa kwa usimamizi wa viongozi wa serikali, maofisa elimu na mbunge na kwamba maktaba zinaendelea kujengwa na nyingine zimekamilika na zinatumika kwenye baadhi ya shule na pia kazi ya kuboresha na kujenga nyumba za walimu na vyoo vipya inaendelea.



## HABARI DODOMA

# Ujenzi barabara mji wa kiserikali uko pazuri

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

UJENZI wa barabara za kiwango cha lami katika mji wa serikali Mtumba, jijini hapa zenye urefu wa kilomita 51.2 umefikia asilimia 56.

Katibu wa Kuratibu Serikali Kuhamia Dodoma na Uratibu wa Ujenzi wa Mji wa Mitumba, Meshack Bandawe, alibainisha hayo jana wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara hizo.

Alisema kazi hiyo inafanywa kwa gharama ya Sh. bilioni 88.1 na inatekelezwa na mkandarasi kutoka China na inatarajiwa kukamilika ifikapo Julai 31, mwaka huu.

"Sasa hivi kinachoendelea ni ujenzi wa barabara za lami zinazozunguka ndani ya mji wa serikali na ujenzi huu umefikia sehemu nzuri na ikifika Julai mwaka huu utakuwa umekamilika," alisema.

Alisema ujenzi huo unahusisha barabara za njia mbili za urefu wa kilomita 22.4 na zenye njia moja zenye urefu wa kilomita 28.8 pamoja na miundombinu mingine kama maji, umeme, gesi, usambazaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), zimamoto na uokoaji, maduka makubwa pamoja na huduma za treni.

Katika hatua nyingine, alisema ujenzi wa ofisi awamu ya pili utaanza baada ya kupata kibali hivi karibuni.

Mradi huo ulizinduliwa na Rais John Magufuli Machi 2019 na unasimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

# Mabinti kaya maskini waanza kukingwa VVU

**Na Augusta Njoji,** BAHI

TUME ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), imetangaza mkakati wa kitaifa wa kuwaweka kambini wanafunzi wa kike kutoka kaya maskini nchini, kuwapa mafunzo ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati akifungua kambi ya majaribio wilayani Bahi, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera na Uratibu), Dorothy Mwaluko, alisema majaribio yatasaidia serikali kuendesha kambi za namna hiyo kwenye halmashauri nyingine nchini ili kuwalinda wasichana.

Katika kambi hizo watafundishwa stadi za maisha, masomo ya Sayansi na Hisabati, ili wafanye vizuri kwenye masomo hayo, wajitambue na kujiamini.

**Kwa sasa mradi huo unatekelezwa katika halmashauri 10 za Dodoma, Singida na Morogoro na mikoa ya Tanga na Geita imeongezwa kwenye mradi huo.**

"Kambi hii ni ya majaribio kwa wanafunzi wasichana balehe 105 kutoka shule 18 kutoka kwenye kaya maskini zilizo chini ya mpango wa Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), tunajipanga kufanya kambi hizi kwenye halmashauri nyingine zote," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema wamepanga kuwa na utaratibu wa kuwa na kambi za wanafunzi wasichana balehe 1,324 walioko shuleni kila baada ya miezi sita.

Vilevile, alisema Bahi kuna mfuko wa elimu wa halmashauri ambao utawaendeleza kielimu hadi chuo kikuu.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Mwitikio wa Taifa, TACAIDS, Audrey Njelekela, akifafanua kuhusu kambi hiyo, alisema ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa Timiza Malengo unaowalenga wasichana balehe na wanawake vijana waliopo ndani na nje ya shule kutimiza malengo yao.

Alisema kwa sasa mradi huo unatekelezwa katika halmashauri 10 za Dodoma, Singida na Morogoro na mikoa ya Tanga na Geita imeongezwa kwenye mradi huo.

Mratibu wa mradi huo wa kambi, Salum Kilipamwambu, alibainisha kuwa utafiti wa elimu ya sekondari unaonyesha kuwa wanafunzi wa kike wa sekondari wamekuwa wakishindwa kuhitimu masomo yao kwa kukosa uelewa na kutojitambua na kujiamini.

Mwanafunzi kutoka Sekondari ya Kigwe, anayeshiriki mpango huo Mwajuma Hamisi, alisema mafunzo hayo yamesaidia kujitambua, kujiamini na kuongeza weledi kwenye masomo ya sayansi na hisabati.



Mjasiriamali ambaye ana ulemavu wa viungo mkazi wa Chigongwe jijini Dodoma, akipanga bidhaa zake kando na ukuta wa Kanisa Kuu la Anglikani kwa ajili ya kusubiri wateja wake. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TALIRI yapendekeza ufugaji mbuzi mzaa mapacha

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

KITUO cha Utafiti wa Mifugo Kongwa (TALIRI) kimewashauri wanaofuga mbuzi kufuga aina ya 'malya' mwenye sifa ya kutoa maziwa mengi, nyama kwa wingi na anayezaa mapacha.

Kwa mujibu wa mtafiti wa TALIRI Kongwa, Christopher Mtangwe, mbuzi hao ni chotara wenye mchanganyiko wa jamii za kienyeji na aina ya 'boer' kutoka Afrika Kusini.

Akielezea faida ya mbuzi huyo kwa waandishi wa habari na maofisa wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) waliotembelea kituo hicho, Mtangwe alisema moja ya faida kubwa ya mbuzi huyo ni kuvumilia ukame.

"Pia ana sifa ya kuzaa mapacha, wanazaliwa hata hadi watatu na kuendelea," alisema mtafiti huyo.

Aliwaambia kuwa faida hizo zinamwezesha mfugaji kuuza maziwa na nyama kwa jamii inayomzunguka na kuongeza idadi ya mifugo kutokana na kuzaa mapacha mara nyingi.

Aliwashauri wafugaji hao kupanua wigo wa kufuga mbuzi hao ambao watakwenda kubadilisha aina ya ufugaji.

Alisema tayari wameanza kuwasambaza katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kuwa wafugaji wanafanya ufugaji wenye tija ambao utaleta matokeo chanya kwa wafugaji.

Aliishukuru serikali kupitia COSTECH kwa kutoa fedha kwa ajili ya watafiti wa mifugo na miradi mingine ya maendeleo ili kuleta matokeo chanya kwa wafugaji na wakulima pamoja na kwa taifa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TALIRI Kongwa, Dk. Wilfred Munisi, alisema kituo kinafanya jitihada za kuwaelimisha wafugaji namna ya kufuga mifugo yao ili iwaletee faida.

Alisema teknolojia ya kutumia mbuzi chotara ina manufaa makubwa kwa mfugaji kwa sababu wanavumilia magonjwa, ukame lakini kukua haraka na kuzaa mapacha hata zaidi ya mara tatu.

Alisema watafiti wataendelea kufanya kazi hizo tofauti ili kuhakikisha mkulima na mfugaji wanapata elimu iliyo bora ambayo itawasaidia kuendesha ufugaji wa kisasa na wenye tija na kukuza uchumi na afya zao.

Mfugaji Michael Madeje, alisema ufugaji unalipa endapo mfugaji atafuga kulingana na maelekezo ya wataalamu.

Alisema hivi sasa taifa lipo katika uchumi wa kati na wafugaji wanapaswa kubadilika ili kuendana na mazingira ya sasa ya kupiga hatua kwa kile wanachokifanya.



# Viongozi 4 wasimamishwa kazi madai ya rushwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

VIONGOZI wanne wa vijiji katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wamesimamishwa kazi kwa tuhuma za kupokea rushwa kutoka kwa wafugaji na kuruhusu makundi ya mifugo kutoka maeneo mengine kuhamia kwenye vijiji hivyo kinyume cha sheria.

**Wapo wengine tunaendelea kuwachunguza kwa tuhuma za aina hiyo na tukibaini kuwa kuna ukweli, tutawachukulia hatua kama wenzao ili kukomesha tabia hii ambayo ina madhara makubwa kwenye wilaya yetu.**

Waliosimamishwa ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Kambikatoto, Saimon Maganga, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Erick Msola, Mwenyekiti wa Kijiji cha Sipa, Maulid Migamba, Ofisa Mtendaji, Laurent Namwinga na Ofisa Ugani wa Kijiji cha Kambikatoto, Samwel Lyeme.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Saimon Mayeka, alisema mbali na viongozi hao kupokea rushwa na kuruhusu mifugo kuingia kwenye vijiji vyao, pia wamehusika kwenye uuzaji wa maeneo makubwa ya ardhi kwa wageni.

"Wapo wengine tunaendelea kuwachunguza kwa tuhuma za aina hiyo na tukibaini kuwa kuna ukweli, tutawachukulia hatua kama wenzao ili kukomesha tabia hii ambayo ina madhara makubwa kwenye wilaya yetu," alisema Mayeka.

Alifafanua kuwa serikali ya wilaya hiyo haizuii wafugaji kutoka kwenye maeneo mengine kuingia wilayani humo, lakini inawataka wafuate taratibu za kisheria badala ya kuingia kinyemela.

Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Chunya, Dk. Benedict Matogo, alisema uingizaji wa mifugo kienyeji wilayani humo una madhara makubwa ikiwamo kusambaa kwa magonjwa ya mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine.

Alisema vilevile, unasababisha ongezeko la mifugo na kusababisha maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo kutokidhi mahitaji hali inayosababisha kuibuka migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Alisema baadhi ya wafugaji wanaingia kwenye maeneo ya vijiji kwa nguvu na kusababisha uvunjifu wa amani kwenye maeneo hayo ndiyo maana serikali iliamua kuweka utaratibu.

"Wakati mwingine tukiamua kuwafuatilia wafugaji hawa wanaanza kutumia nguvu, sasa tunatakiwa kuchukua hatua kali zaidi kuwadhibiti maana ni hatari sana mwingiliano huu ambao haufuati utaratibu," alisema Dk. Matogo.

Baadhi ya wafugaji wilayani humo waliipongeza serikali kwa uamuzi huo wakidai kuwa utawasaidia kupunguza migogoro.

Mmoja wa wafugaji, Josia Mwankale, alisema wafugaji wapya wanapoingiza mifugo kwenye vijiji vyao wanakuwa hawazijui taratibu za vijiji hivyo na kwamba wakiingia wanakuwa na taratibu za kwao ambazo zinakuwa kinyume na wenyeji.

Baadhi ya wakulima wa vijiji vya wilaya hiyo walisema wafugaji wamekuwa wakiingiza mifugo kwenye mashamba yao na kulisha mazao na kusababisha migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mmoja wa wakulima hao, Anthony Jeremiah, alisema baadhi ya maeneo wananchi wamekuwa wakikumbwa na njaa kutokana na mazao yao kuliwa na mifugo.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon (katikati), akikagua moja ya madaraja yaliyojengwa kwenye mradi wa barabara ya Chunya- Makongolosi juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbunge kuvalia njuga unyanyasaji wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** MOMBA

MBUNGE wa Jimbo la Momba, mkoani Songwe, Condesta Sichalwe, ameahidi kuingilia kati suala la madai ya wawekezaji kuwanyanyasa wakulima wa Kata ya Kapele ambao wanadai kuny'ang'anywa mashamba yao kimabavu.

Mbunge Sichalwe alipokea malalamiko hayo jana wakati wa kikao cha kusikiliza kero za wananchi na moja ya hoja zilizotolewa na wananchi hao ni kunyanyaswa na wawekezaji ambao hujimegea mashamba ya mpunga kimabavu.

Alisema anakwenda kushughulikia kero hiyo kwa kushirikiana na vyombo vya sheria na atakayebainika atachukuliwa hatua.

Aliwaomba wakulima wa Kata ya Kapele, kutokubali kuachia maeneo yao ya kilimo kwa madai kuwa wanahaki na waendelee na shughuli za kilimo kama kawaida, huku akiwaomba watendaji na viongozi wengine kushughulikia suala hilo.

"Nimepokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa Kapele, kudai kunyanyaswa na baadhi ya watu ambao wanajiita wawekezaji, wanajimegea maeneo makubwa ya mashamba bila kufuata utaratibu, halafu wanawageuka wananchi wangu wakikutwa kwenye maeneo hayo wanapigwa na kutishiwa," alisema Sichalwe.

Aliliomba Jeshi la Polisi kushughulikia suala hilo ikiwamo kuwakamata na kuchukua hatua kwa wawekezaji wote wanaodaiwa kuwanyanyasa kwa vipigo na kuwany'ang'anya mashamba wakulima.

Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Momba, Twist Maulid, aliwaomba wananchi wa Kapele kutofumbia macho vitendo hivyo vya ukatili na kutokubali kurubuniwa kwa vipande vya fedha ili kuachia ardhi yao.

# Mil. 500/- kuongeza majengo ya afya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imetoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kuongeza majengo kwenye Kituo cha Afya cha Igawilo, kilichopo katika Bonde la Uyole jijini Mbeya kwa lengo la kukipandisha hadhi kuwa hospitali ya wilaya.

Akizungumza juzi na wananchi wa Kata ya Igawilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema fedha hizo zilitolewa kupanua kituo cha afya ili kipandishwe hadhi kuwa hospitali ya wilaya.

Alisema ujenzi umeanza kwa ajili ya kukarabati na kuongeza majengo mengine muhimu ya kutolea huduma na unatarajiwa kukamilika kabla ya Septemba, mwaka huu.

"Serikali tayari imekwisha ingiza fedha Sh. milioni 500 kwenye akaunti ya halmashauri, fedha za ujenzi wa kituo hicho cha afya lengo letu tunakipandisha kiwe hadhi ya hospitaji ya jiji tutahakikisha miundombinu yote ya kutolea huduma inakuwapo, tunasisitiza ujenzi huo ukamilike kwa wakati kufika Septemba mwaka huu," alisema Chalamila.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya, walisema uamuzi wa serikali kukipandisha hadhi kituo hicho cha afya wameupokea wakiamini kuwa hospitali hiyo itakuwa ni msaada mkubwa kwa wananchi wa Bonde la Uyole na maeneo jirani.

Alisema kwa sasa wanaendelea kupata huduma kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya licha ya kutumia umbali mrefu.

Flora Fumbo na wenzake waliahidi kushirikiana na mafundi wanaojenga hospitali hiyo ili kazi hiyo ikamilike haraka na hatimaye wapate huduma bora za kiafya jirani na makazi yao.



# SMZ yaanza kushughulikia ukosefu ajira

**Na Hawa Aabdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali inatambua ukubwa wa tatizo la ajira linalowakabili vijana na wameanza kuchukua hatua ikiwa ni utekelezaji wa ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu.

Alitoa kauli hiyo juzi katika kilele cha matembezi ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), yaliofanyika Uwanja wa Mao Zedong, jijini hapa.

Alisema wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu uliopita, CCM kiliahidi kukabiliana na tatizo la ajira linalowakabili vijana na kwamba ahadi hiyo imeanza kutekelezwa kupitia wawekezaji walioanza kuja nchini kuwekeza katika miradi mbalimbali, ikiwamo sekta ya utalii.

Dk. Mwinyi alisema serikali inakusudia kuendelea kuwajengea uwezo vijana kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi pamoja na kuimarisha shughuli za ujasiriamali ili kuwa katika mazingira bora ya kujitegemea.

**Vijana ndiyo nguzo muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, kwa kuzingatia kuwa wao ndiyo msingi muhimu wa uzalishaji.**

Hivyo, aliwataka vijana kujituma kwa kufanyakazi kwa bidii na kuondokana na dhana ya kuchagua kazi ili waweze kupata mafanikio.

Alisema jamii ya Wazanzibari inakabiliwa na matatizo mbalimbali, ikiwamo ya kutowajibikaji kwa watendaji wa serikali, na kuwataka vijana kujitambua na kuisaidia katika mapambano hayo na kufanya ushawishi kwa vijana wenzao ili waweze kuepuka vitendo viovu.

Kuhusu kaulimbiu ya matembezi hayo 'Uzalendo na uwajibikaji ni msingi wa maendeleo ya Zanzibar kufikia Uchumi wa Buluu', Dk. Mwinyi alisema amevutiwa na ujumbe huo kwa kuwa unakwenda sambamba na malengo ya serikali kuhakikisha inapata maendeleo ya haraka ya kuchumi kupitia uchumi wa buluu.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi alisema matembezi hayo ni kielelezo kuwa vijana wa CCM wanathamini Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964, ikiwa mwanzo wa safari ya kuzaliwa kwa Muungano wa Tanzania.

Alisema vijana ndiyo nguzo muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, kwa kuzingatia kuwa wao ndiyo msingi muhimu wa uzalishaji.

Alieleza kuwa Mapinduzi ya 1964 yalifungua milango ya kujitawala na kuleta uhuru, hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kufanya kazi.

Alisema mshikamano ndiyo utakaofanikisha amani na utulivu nchini na ndoto ya maendeleo na kutoa rai kwa wananchi kudumisha amani iliyopo.

Dk. Mwinyi aliwapongeza UVCCM kwa kuandaa matembezi hayo kila mwaka katika kipindi kama hicho cha shamrashamra za sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema serikali imejipanga kuzipitia upya sheria zote zenye utata ama kukinzana, huku akiahidi kuendelea kuwapa fursa za uteuzi vijana katika ngazi mbalimbali.

Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Kheri James, alisema Jumuiya hiyo inatambua dhima iliyonayo katika mapambano dhidi ya vitendo vinavyorudisha maendeleo ya nchi na kubainisha kuwa inaunga mkono kwa hali na mali juhudi za serikali.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano Jumuiya hiyo imekuwa ikiendesha programu mbalimbali, ikiwamo ya kuboresha makazi pamoja kuwajengea uwezo vijana wake ili hatimaye iweze kuwa na viongozi bora.

Naibu Katibu Mkuu UVCCM Zanzibar, Mussa Haji Musa, alisema matembezi hayo yalihusisha vijana 750 kutoka mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar na kuzinduliwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, Januari 5, mwaka huu, katika Kijiji cha Pwani Mchangani.

## Maalim Seif awataka Waislam kujiandaa kiimani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, amewataka waumini wa dini ya Kiislamu kujiandaa kiimani kwa kuwa kila mmoja ipo siku ataondoka duniani.

Alisema katika imani ya dini ya Kiislamu kila mwanadamu kuna siku atarudi kwa muumba wake na kwamba ni vyema kufanya mambo yanayompendeza Mungu kwa kufuata misingi na imani ya dini hiyo.

Aliyasema hayo katika hafla ya uzinduzi wa sehemu rasmi ya kuoshea na kukafini maiti eneo la Ukutani kwa Bakathir, Jimbo la Malindi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Kituo hicho ambacho kipo chini ya Taasisi ya Annour Islamic Centre, kimejengwa kwa ufadhili wa kikundi cha Tears of Joy kilichopo nchini Uingereza.

Maalim Seif alimshukuru kiongozi wa bodi ya Annour Islamic Centre, Sheikh Hamed Rashid Hikman na wenzake kwa kuzalisha wazo hilo lenye manufaa katika jamii.

Vilevile, alimshukuru kiongozi wa kikundi hicho, Sheikh Suleiman Ahmed Sadiq na wanakikundi wenzake kwa kuwezesha ujenzi huo mpaka kufikia hatua ya matumizi.

Aliwataka Wazanzibari wengine wanaoishi nje ya nchi kuisaidia Zanzibar katika nyanja mbalimbali ikiwamo mambo ya kijamii.

Pia aliwasisitiza wananchi wa Malindi na viunga vyake kukitumia kituo hicho kama madhumuni yanavyotaka pamoja na kuwataka wazazi kuwahimiza vijana wao kuwa ni sehemu ya kufanya shughuli hizo.




Watalii mbalimbali waliowasili Visiwani Zanzibar, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amaan Karume, juzi. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

## Watalii kutoka Oman, Urusi wamiminika Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

IDADI kubwa ya watalii imeendelea kumiminika visiwani hapa baada ya juzi Uwanja wa Ndege wa Abeid Amaan Karume kufurika watalii hao kutoka mataifa mbalimbali wakiwamo wa Urusi na Oman.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Mulhat Yussuf Said, alisema ujio wa watalii hao unatokana na juhudi za serikali ikiwamo kuboresha huduma za uwanja huo pamoja jitihada za mapambano dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Alisema wakati nchi ikikabiliwa na ugonjwa wa corona mashirika mbalimbali ya ndege yalisitisha safari, lakini kwa sasa mashirika hayo ikiwamo Oman yameanza kufanya safari zake visiwani Zanzibar pamoja na kuleta watalii. Alisema idadi ya watalii inazidi kuongezeka baada ya nchi kutokuwa na maradhi ya corona licha ya baadhi ya mataifa ulimwenguni yakikabiliwa na janga hilo.

Alisema watalii wote wanaoingia na kutoka Zanzibar lazima serikali ijiridhishe kwa kufuata miongozo yote ya afya, pamoja na kupima ugonjwa huo na kukabidhiwa cheti cha uthibitisho.

Aliwataka wafanyakazi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuongeza juhudi kwa kuwahudumia wasafiri wanaofika kiwanjani hapo, ili wageni wanaofika Zanzibar wasipate usumbufu.

Ofisa huyo alisema zaidi ya mashirika matano ya ndege yamewasili Zanzibar yakiwa na watalii zaidi ya 500, hatua iliyowezesha serikali kupata mapato yatokanayo na sekta hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## NAFASI YA KAZI

**ANATAFUTWA DEREVA,** Anatafutwa dereva wa kike mwenye uzoefu wa kuendesha Magari Mjini Dar es Salaam. Mwenye nia na kazi hiyo apige namba **0784691605/0715691605.**

## OFISI ZA MATANGAZO

Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;12/2021**

**Ombi la FIDEA DICK MWANDETELE,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ANANGUSYE DICK MWANDETELE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/02/2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 07/01/2021.

Tarehe 7/1/20.21
Sahihi ya Hakimu
Mahakama ya Mwanzo Mjini

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NORBERT MUSSA NJELEKELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **T BETTER** Yenye namba za usajili **T 334 BUS.** Chassis No. **LZEPCKLA506816759.** Engine **No.ZJ162FMJB2516795.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/RB/129/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**WILAYA YA SINGIDA – SINGIDA**

**SHAURI LA MADAI NA. 01/2021**

**MDAI: BENEDICT HAMBANAYE**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: JUDITH AUGOSTINO**

**WITO KWA JUDITH AUGOSTINO KUPITIA KWA MWENYEKITI WA MTAA KIMPUNGUA – SINDIDA**

Unaamriwa na Jamhuri uhudhurie mbele ya Mahakama hii tarehe 14 mwezi 01 mwaka 2021 saa 2:30 asubuhi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa Mahakama leo tarehe 15 Mwezi 01 Mwaka 2021.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI-SINGIDA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI DAR ES SALAAM**
**KISUTU**

**CIVIL CASE NO. 202/2019**

**FAST JET AIR FORCE ONE................WADAI**
**Dhidi ya**
**Mwantumu Mohamed**
**Robby Magori**
**Monica De Mello**
**Flaviana**
**Jack Mgonja**
**Enna Lutengano**
**Halima Rajabu**
**Mariam Saroga**
**Mary Swai**
**Sadra**
**Sharifa Mataka..................WADAIWA**

**Kwa: Mwantumu Mohamed, Robby Magori, Monica De Mello, Flaviana, Jack Mgonja, Halima Rajabu, Mariam Saroga, Mary Swai, Sadra, Sharifa Mataka, Popote mlipo.**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo mnahitajiwa/unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 21 Mwezi Februari, 2021 saa 7:00 mchana mbele ya Mhe. Ruboroga, PRM.
ANGALIA: Kama hamtahudhuria/hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itaweza kutoa hukumu bila ya uwepo wako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 08 Mwezi Januari, 2021.

HAKIMU MKAZI/ MKUU/MWANDAMIZI
DAR ES SALAAM - KISUTU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO (W)-BOMANI**

**WILAYA YA IRINGA MJINI**

**KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA NDOA. 11/2021**

**MDAI.....PIUS FRANCIS MLANGWA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA.....MGALA JUMA MAGILI**

**Shauri tajwa hapo juu limefunguliwa katika mahakama hii, na mdai dhidi yako mdaiwa.**

Hivyo unaamriwa wewe mdaiwa mpopote pale ulipo kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 13/01/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa kwaajili ya kujibu madai hayo. Na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako kwaajili ya kujitetea pamoja na hati zote zinazohusu shauri hilo. Usipofika bila taarifa shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 04/01/2021.




UZA, CHENYE THAMANI KUBWA KWA KUTANGAZA NASI
KWA BEI POA TUPIGIE MOB: +255 - 745 700 710

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Mwanafunzi akiri kuiua familia akidai wafuasi wa shetani

**Nairobi, KENYA**

MWANAFUNZI wa chuo kikuu nchini Kenya, Simon Warunge, amekiri kwa polisi na kutoa taarifa namna alivyopanga na kuwaua watu watano wa familia yake, akiwamo baba na mama yake.

Vyombo vya habari vya nchini humo, vimeripoti kuwa Warunge ambaye ana umri wa miaka 22, alidai alitumia chuma kumgonga mama, kaka, baba na binamu yake kabla ya kuwachoma visu.

Mwanafunzi huyo, aliwaambia polisi kuwa wazazi wake walikuwa wafuasi wa shetani na makatili, limeripoti gazeti la The Star.

Alisema kuwa walikuwa wanamchukia na kumsema akiwa hayupo, imeripoti televisheni ya Citizen, nchini humo.

Dada zake wawili, ambao walikuwa wamerejea shuleni walinusurika na shambulio hilo.

Mama yake, alikuwa ni muuguzi wa kisaikolojia nchini Kenya na baba yake alikuwa muuguzi nchini Marekani, aliwasili nchini Kenya kwa ajili ya sherehe za Krismasi kabla ya mauaji hayo.

Wachunguzi wameanza uchunguzi upya kuhusiana na mauaji mengine ambayo yalitokea katika ndugu wengine wa familia hiyo.

Polisi pia wamemkamata mpenzi wa mshukiwa huyo, ambao walifikishwa mahakamani jana, Jumatatu.

*BBC*




Maofisa wa Jeshi la Majini nchini Indonesia, wakibeba sehemu ya mabaki yanayoaminiwa ya ndege ya Shirika la Sriwijaya Air Boeing 737, SJ-182, iliyopotea kwenye rada na abiria 62 kuelekea kisiwa cha Borneo, mwishoni mwa wiki. **PICHA/BBC**

# Malawi yaanza siku 21 kufunga, kuomba dhidi ya corona

**Lilongwe, MALAWI**

RAIS wa Malawi, Lazarus Chakwera, amesema kutokana na ongezeko la maambukizi ya virusi vya corona, nchi itaanza kufanya maombi kwa siku 21.

Rais Chakwera alisema takwimu zinazoonesha ongezeko la karibuni la maambukizi ya virusi hivyo, nchini mwake, zinahuzunisha.

Katika hotuba ya Jumapili mwishoni mwa wiki, kwa njia ya redio alitangaza anaanza siku 21 za kufunga na kumwomba Mungu, aepushe janga ambalo limeongezeka tena.

Wataalamu wa afya wanasema, hali iliyopo nchini humo inahitaji zaidi ya maombi ya sala.

Malawi hivi karibuni imeshuhudia ongezeko katika kesi za virusi vya corona.

Alhamisi wiki iliyopita, nchi hiyo ilikuwa ikithibitisha kesi nyingi za Covid-19 kuwahi kurekodiwa.

Jumamosi, Malawi ilirekodi kesi 381 za virusi vya corona na vifo 12 idadi kubwa siku moja tangu iliporekodi kesi tatu za kwanza, Aprili, mwaka jana.

Chakwera alisema hivi sasa ni wakati kwa kila mtu nchini humo kurudia utekelezaji wa masharti ya kuzuia Covid-19.

"Kasi ambayo virusi vimekuwa vikienea tangu Krismasi inasumbua sana. Maambukizi mapya 66 yalithibitishwa kati ya siku ya Krismasi na siku inayofuata yaani Boxing Day.

Na katika wiki mbili zilizopita tangu hapo, zaidi ya maambukizi mapya 1,500 yamethibitishwa ambayo ni wastani wa maambukizi mapya zaidi ya 120 kila siku, ambayo yanaweka shinikizo kubwa katika mfumo wetu wa afya na wafanyakazi wa afya, hali hii haiwezi kuruhusiwa kuendelea." Alieleza kuwa, ameziagiza wizara za usalama wa ndani na afya kuongeza utekelezaji wa miongozo ya kujikinga na ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona.

Wizara ya Afya nchini Malawi, ilisema kiasi cha watu 500 waliorudi kutoka Afrika Kusini Jumamosi, wametengwa katika kituo kimoja, huko Blantyre kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya Covid-19.

*VOA*

## Uchaguzi Mkuu Uganda kufanyika kesho kutwa

**Kigali, UGANDA**

UCHAGUZI mkuu nchini Uganda, unatarajia kufanyika Alhamisi, wakati hofu ikiendelea kutanda kutokana na kampeni nchini humo kutawaliwa na maofisa wa usalama, kukabiliana na wagombea wa upinzani na wanahabari.

Pia uchaguzi huo unakabiliwa na janga la virusi vya corona.

Tume ya uchaguzi imetoa angalizo kwa wagombea wote kuzingatia taratibu za afya kuepusha kuenea kwa maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi hivyo.

Rais Yoweri Museveni, ambaye anawania muhula mwingine, anakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa hasimu wake kisiasa mgombea wa upinzani, Robert Kyagulanyi almaarufu Bobi Wine.

Museveni, aliingia madarakani baada ya kutoka katika mapigano ya msituni mwaka 1986 na anatambulika kuwa kiongozi amedumu kwa muda mrefu zaidi barani Afrika.

Rais huyo mwenye miaka 76, ameweza kulifanya taifa hilo kuwa na amani kwa muda mrefu na kuleta maendeleo ambayo wengi wanafurahia.

Pia ameimarisha utawala wake kwa kuhamasisha utu na ushirikiano, kutoa ajira, kuruhusu kuanzishwa kwa taasisi huru na kuwatenga wapinzani.

Bobi Wine, ni mwimbaji ambaye jina lake halisi ni Robert Kyagulanyi, ameendelea kukumbana na changamoto kadhaa na askari.

Mbunge huyo ambaye nyota aliyeweza kuvuta umati mkubwa wa vijana, alikumbana na masaibu kadhaa katika kampeni zake.

Katika kampeni zake polisi walimkamata na kumfunga, wafuasi wake walipigwa mabomu ya machozi na kupigwa risasi kwa kuwa walikuwa wanaenda kinyume na masharti dhidi ya corona.

Wakati wa kampeni, waandamanaji 54 waliuawa wakati Bobi Wine aliposhikiliwa na polisi na wengine wengi wanaaminika kuwa walipigwa risasi.

Miaka 12 iliyopita, Bobi Wine alikuwa akijulikana kwa kuimba nyimbo zinazoeleza maisha ya watu maskini, yeye mwenyewe akiwa amezaliwa na kukulia katika mazingira ya kimaskini huko Kamwokya.

Jambo hilo, ndilo lililompa umaarufu mkubwa miongoni mwa wananchi wa taifa hilo, ambao wengi wao ni maskini.

**RFI**

## Maporomoko ya ardhi yaua 13 Indonesia

**Java, INDONESIA**

WATU 13 wamefariki dunia katika maporomoko ya ardhi yaliyosababishwa na mvua kubwa kwenye kisiwa cha Java cha Indonesia.

Maporomoko hayo ya ardhi yalitokea katika kijiji cha Cihanjuang, Magharibi mwa kisiwa hicho.

Jitihada za kutafuta na kuokoa zinaendelea katika mkoa huo, huku mvua ikitarajiwa kuendelea kwa siku chache zaidi.

*TRT*



# CONTE AJITETEA BAADA YA SARE

**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte amejitetea kwa kufanya mabadiliko ya wachezaji dakika za majeruhi wakati Inter Milan wakilazimishwa sare ya mabao 2-2 na Roma, Jumapili.

Nerazzurri hao walionekana kama wangeondoka na pointi zote tatu kwenye mchezo huo uliopigwa dimba la Olimpico, lakini Gianluca Mancini aliwasaidia katika dakika ya 86.

Lorenzo Pellegrini aliwaweka mbele Roma katika kipindi cha kwanza, lakini mabao mawili ndani ya dakika saba kutoka kwa Milan Skriniar na Achraf Hakimi yakawapa uongozi Inter.

Conte aliwatoa Hakimi, Lautaro Martinez na Arturo Vidal kabla ya Mancini kufunga bao hilo la kusawazisha, na kocha wa Inter, ameelezea kwa nini alifanya mabadiliko hayo.

Alisema: “Vidal aliomba kutolewa baada ya kuumia, Lautaro alifanya mengi kwa dakika 75, nikamtoa.

“Hakimi pia alikimbia sana na alikuwa anapoteza mipira muhimu. Huu ni mchezo wa tatu ndani ya siku saba. Inter lazima iwe na kikosi muhimu ili kufanya matokeo kuwa mazuri.

“Sikuona sababu yoyote ya kutowatumia wachezaji waliokuwa benchi, ndio maana nikawapa nafasi. Lakini hiyo siyo sababu ya kutoka sare, maana mchezo tulishaumiliki kwa kipindi kirefu.”

## CHELSEA SASA YAJITOSA SAINI YA UPAMECANO

**MANCHESTER, England**

MAJALIWA ya mlinzi wa RB Leipzig, Dayot Upamecano, yanaonekana kuwa shakani klabuni hapo na kuna uwezekano mkubwa akatua kwenye Ligi Kuu England.


Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa anatajwa kama mmoja wachezaji wenye vipaji vya hali ya juu barani Ulaya na amekuwa nguzo kubwa kwa Leipzig ambayo imeruhusu mabao 12 tu katika mechi 15 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu huu.

Upamecano mwenye umri wa miaka 22, anaonekana kwamba anaweza kuuzwa kwa bei kubwa, huku ikionekana wazi kwamba, anaweza kutua England.

Kwa mujibu wa Sky Sport, Chelsea imeingia kwenye mbio za kuwania saini ya nyota huyo, wakati kocha wake, Frank Lampard akiwa kwenye wakati mgumu kutokana na matokeo mabaya ya kikosi hicho.

Huku Thiago Silva mwenye umri wa miaka 36 na Kurt Zouma wakiwa ndio chaguo lake la kwanza, Lampard anaonekana hawaamini Antonio Rudiger, Andreas Christensen na Fikayo Tomori.

Kwa mujibu wa ripoti, Chelsea ipo tayati kutoa kiasi cha euro milioni 50 ili kupata saini ya mchezaji huyo.



## IBRAHIMOVIC ASHAURIWA KURUDI TENA TAIFA SWEDEN

**ROME, Italia**

DEJAN Kulusevski amemshauri nyota wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic kurudi kuichezea Sweden kwenye michuano ya Euro 2020.

Michuano hiyo ya Mataifa ya Ulaya iliyokuwa ifanyike mwaka jana, iliahirishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona na sasa itafanyika mwaka huu.

Ibrahimovic hajaichezea timu ya Taifa ya Sweden kwa zaidi ya miaka minne baada ya kutangaza kustaafu mwaka 2016.


Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 39, ambaye ni mfungaji wa wakati wote wa Sweden akiwa na mabao 62 katika mechi 116 - alidokeza kuwa yupo tayari kurudi kuichezea timu yake hiyo ya taifa baada ya kuwa na muda wa kuvutia pale Milan.

Na sasa nyota huyo wa Sweden na straika wa Juventus, Kulusevski amezungumzia kuhusu kutaka kurudi kwa Ibrahimovic kwenye kikosi cha taifa.

“Tunawasiliana mara kwa mara. Ni mchezaji anayenivutia sana, ni wachache wanaoweza kufanya kile alichokifanya hadi sasa,” alisema Kulusevski akiiambia Sky Sport Italia kuhusu Ibrahimovic, ambaye amefunga mabao 10 kwenye Ligi msimu huu na 11 katika mashindano yote aliyowachezea Milan.

“Natumaini atarudi kuichezea timu ya Taifa ya Sweden kwenye mashindano ya Euro. Litakuwa jambo zuri sana kwangu kucheza naye.”

HABARI MICHEZO



# CAMAVINGA

## AFUNGUKA KUWANIWA REAL MADRID

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA Eduard Camavinga amekiri kwamba "ni vizuri pale klabu kubwa zikivutiwa na wewe" wakati huu akiwa anahusishwa na mabingwa wa La-Liga, Real Madrid.

Camavinga amekuwa akisita kuondoka katika klabu ya Rennes ya Ligi Kuu Ufaransa kwenda Real Madrid, ambao wamekuwa wakitamani kuinasa saini yake.

Mbingwa wa Ufaransa, Paris Saint-Germain, Juventus na Manchester Uited zote pia zimetajwa kuwania saini ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 18.

"Ndiyo ni vizuri sana kama unatakiwa na klabu kubwa," Camavinga aliiambia Canal wakati huu uvumi ukizidi kuwa mkubwa kuhususu hatima yake.

"Lakini mimi natuliza kichwa. Bado niko Rennes, tutasubiri mpaka mwisho wa msimu.

"Tutakutana mezani na tutapima hasara na faida kisha tutaamua."


Camavinga alicheza mchezo wa kwanza kwa timu ya vijana ya Rennes mwaka 2019 na haraka sana aliweza kuonyesha kipaji chake na kikaonekana.

Mfaransa huyo amefunga bao moja na kutoa pasi moja ya mwisho katika mechi 17 za ligi msimu huu na timu yake ipo katika nafasi ya tano alama saba nyuma ya viongozi wa Ligue 1, Lyon baada ya kwenda nao sare ya mabao 2-2 Jumamosi.

## DORTMUND YAMGOMEA BRANDT

**DORTMUND, Ujerumani**

KLABU ya Borussia Dortmund imetoa tamko kuhusu tetesi za usajili wa Julian Brandt.



Brandt mwenye umri wa miaka 24, anahusishwa kutimkia Ligi Kuu England, ingawa bado anamkataba na klabu ya Borussia Dortmund hadi mwaka 2024.

Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Michael Zorc, amenukuliwa akisema, "sitaki kujibu tetesi za usajili zilizotengenezwa na vyombo vya habari. Hadi sasa, Brandt ni mchezaji wetu na hatuna mpango wa kuachana naye.

"Kwa ujumla, tunaangalia mambo mengi hasa uchumi ambapo hali si nzuri kwa sasa kutokana na janga la COVID-19.

"Lakini ninaweza kusema tena, hakuna ofa iliyotufikia mpaka sasa."



## UNITED YAJITOSA KUMNASA FAIVRE

**PARIS, Ufaransa**

IMERIPOTIWA kwamba Manchester United ipo tayari kuingia kwenye vita na Klabu ya Paris Saint-Germain, kuwania saini ya kiungo, Romain Faivre.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22 kwa sasa anakipiga ndani ya Klabu ya Brest akiwa amecheza mechi sita na kutupia mabao mawili jambo ambalo limekuwa likiwavutia mabosi wa timu nyingi ikiwa ni pamoja na Man United.

Kiungo huyo raia wa Ufaransa msimu uliopita alikuwa anacheza ndani ya Klabu ya Monaco na usajili wake uliwashtua wengi kwa kuwa uligharimu kiasi cha euro 450,000.

Kiwango ambacho amekuwa akikionyesha ndani ya Brest kimewafanya mabingwa wa Ligue 1, PSG kumtazama kwa karibu ili waweze kuwekeza kwake kwa munufaa ya baadaye kwa mujibu wa Le10Sport ambao wameweka wazi kwamba na Manchester United nao wameonyesha nia ya kuwania saini ya nyota huyo.

Ole Gunnar Solskjaer tayari amemjumuisha kiungo huyo kwenye orodha ya wachezaji ambao anawahitaji huku akiingia kwenye vita na Kocha Mkuu wa PSG, Mauricio Pochettino ambaye anahitaji pia kufanya kazi na kijana huyo.

Faivre, anatajwa kukubalika kwa kocha huyo wa zamani wa Tottenham ambaye ameanza maisha mapya ndani ya PSG.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SANCHO CHAMBO YA HAALAND CITY

●●●Miamba hiyo ya Etihad bado inammiliki nyota huyo wa England kwa asilimia 15, hivyo inataka...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City wanamatumaini ya kumtumia Jadon Sancho kama chambo ya kuwapiku wapinzani wao wa jiji moja, Manchester United kuipata saini ya mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20, amekua akiwaniwa sana na klabu za Ligi Kuu England.

Sancho aliuzwa na Man City kule Dortmund baada ya kukulia katika akademi ya klabu hiyo na amekuwa nyota muhimu kwa kikosi hicho cha Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Nyota huyo wa timu ya Taifa ya England, ambaye amekuwa akitajwa kuwaniwa na klabu ya Real Madrid, sasa Man City inaonekana kwamba wanaweza kumtumia ili kuipata saini ya Haaland.

Haaland ni mchezaji ambaye amekuwa akiwaniwa na klabu nyingi kubwa zikiwamo Man United, Real Madrid, Barcelona, Juventus na Liverpool baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kule Dortmund.

Man City bado inammiliki Sancho kwa asilimia 15 kwenye mkataba wao na Dortmund tangu alipouzwa kule mwaka 2017.

Na wanaamini kwamba, uhusiano wao kibiashara na Dortmund utawawezesha kumshawishi Haaland kujiunga nao.

Sancho alikuwa akihusishwa sana kujiunga na Man United kabla ya kuanza kwa msimu huu wa 2020-21, kabla ya dili hilo kuyeyuka.

## KWA UFUPI

### TIERNEY AWANIWA NAPOLI
NAPOLI wameamua kumfanya mlinzi wa Arsenal, Kieran Tierney kipaumbele chao kwenye usajili ujao, baada ya kumkosa nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, mwanzo mwa msimu huu. ***(Telegraph)***

### FAIVRE HUYOOO UNITED
KLABU ya Manchester United inajiandaa kumenyana na Paris St-Germain katika mbio za kumsaka kiungo wa kati wa Brest na Ufaransa mwenye umri chini ya miaka 21, Romain Faivre. ***(Sun)***

### EVERTON YAMTAKA ANDERSON
EVERTON wanatafakari uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati, Felipe Anderson, mwenye umri wa miaka 27 raia wa Brazil, ambaye yuko Porto kwa mkopo kutoka West Ham United. ***(Teamtalk)***

### CHELSEA HAIMUACHII BARKLEY
CHELSEA hawako tayari kumwachia kiungo wa kati wa England, Ross Barkley, kujiunga na Aston Villa - ambako anacheza kwa mkopo wa msimu mzima -huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, akisaliwa na miaka miwili na nusu kwenye mkataba wake. ***(Birmingham Mail)***

### DIAZ KUONDOKA AC MILAN
MSHAMBULIAJI wa Hispania, Brahim Diaz, anajiandaa kuondoka AC Milan kurejea Real Madrid mara mkataba wake wa mkopo utakapofikia mwisho, licha ya klabu hiyo ya Italia kutaka kubaki na nyota huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Le10Sport)***

### FIKAYO KUTOKWENDA CHELSEA
NEWCASTLE United huenda isiwe maskani mapya kwa mlinzi wa Chelsea, Fikayo Tomori, mwenye umri wa miaka 23, ambaye anajiandaa kuondoka mwezi huu. ***(Chronicle)***

### SANCHO AFUNGUKA KIWANGO
WINGA wa England, Jadon Sancho, amekiri kwamba amekuwa na msimu mgumu kule Borussia Dortmund tangu alipohusishwa na tetesi za kujiunga na Manchester United, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, anaamini kuwa amerejelea katika kiwango chake. ***(Manchester Evening News)***

### FERNANDINHO KUREJEA BRAZIL
WAKALA wa kiungo wa kati wa Manchester City, Fernandinho, amegusia uwezekano wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, kurejea klabu ya Brazil ya Athletico Paranaense mara mkataba wake na City utakapomalizika. ***(Globo Esporte)***

### TUFAN AWINDWA KILA KONA
KLABU ya Fenerbahce inataka kumnunua kiungo wa kati raia wa Uturuki, Ozan Tufan mwenye umri wa miaka 25, kwa pauni milioni 14, huku Crystal Palace, West Bromwich Albion na CSKA Moscow ya Urusi pia zikimtaka mchezaji huyo. ***(Hurriyet)***

### LIVERPOOL YAMTAKA DE BERG
LIVERPOOL imefanya mazungumzo na klabu za Ubelgiji, Ujerumani na Uswisi kuhusu uwezekano wa kumsajili kwa mkopo mlinzi wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 19, Sepp van den Berg. ***(Goal)***

### N'LUNDULU AWANIWA REAL BETIS
MSHAMBULIAJI wa Southampton, Dan N'Lundulu, mwenye umri wa miaka 21, ananyatiwa na Real Betis. Kiungo huyo amebakiza miezi 18 katika mkataba wake wa sasa. ***(TodoFichajes)***

HABARI MICHEZO

# REFA MSTAAFU AWASHUKIA WACHAMBUZI SOKA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya wiki moja ya mitazamo ya baadhi ya wachambuzi wa soka nchini kuhusu penalti ambayo Simba ilipata kwenye mechi dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe, mwamuzi wa zamani nchini na mkufunzi wa waamuzi kwa sasa, Leslie Liunda, ameibuka na kusema ilikuwa halali kwa mujibu wa sheria za soka huku akiwashangaa wanaoipinga.

Mkufunzi huyo, pamoja na mambo mengine, alikuwa akizungumzia juu ya Tanzania kushindwa kutoa hata mwamuzi mmoja kwenye fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) zitakazofanyika nchini Cameroon kuanzia Januari 16 hadi Februari 7, mwaka huu.

Liunda alisema kuna baadhi ya waandishi wa habari na wachambuzi wa michezo wanachangia kuwafanya au kuwaonyesha waamuzi wa Tanzania kuwa ni wababaishaji wakati si kweli.

Alitoa mfano wa mechi ya Simba dhidi ya FC Platinum, baadhi ya waandishi wa habari na wachambuzi wanadai kuwa haikuwa penalti halali, lakini ukweli ilikuwa ni penalti dhahiri kwa sababu aliyemkamata mkono Shomari Kapombe alimshika kuanzia nje na akaendelea kufanya hivyo hadi alipoingia ndani ya eneo la hatari.

"Kanuni inasema kama mchezaji atakuwa amemshika nje ya eneo la hatari na akaendelea kufanya hivyo hadi ndani ya eneo la hatari la penalti, basi itahesabiwa ni penalti," alisema Liunda.

Aliongeza kuwa kama mchezaji huyo angemshika nje ya penalti na kumwachia, halafu mchezaji akaangukia ndani, hapo isingekuwa penalti, lakini mchezaji wa Platinum aliendelea kufanya hivyo mpaka ndani.

Alisema baadhi walipinga kuwa haikuwa penalti, lakini mwamuzi yule alichezesha sawasawa na ndiyo maana amechaguliwa kuwa mmoja wa waamuzi watakaochezesha michuano ya CHAN.

Mwamuzi aliyechezesha mechi kati ya Simba dhidi ya FC Platinum kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumatano iliyopita ni Georges Gatogato kutoka Burundi.

Hata hivyo, mkufunzi huyo aliwataka waamuzi nchini kujiangalia upya na kutokubali kufanya makosa mengi uwanjani, hasa ya kutafsiri sheria.

KATUSUA...




Mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Hassani Mtepa, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 31 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. SportPesa huwapa bonasi washindi kuanzia mechi 10 hadi 12 wa Jackpot kila wiki. **PICHA: SPORTPESA**

# Job atua rasmi Yanga, straika kuanikwa leo

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE baada ya tetesi za muda mrefu, ni rasmi sasa beki kisiki na chipukizi wa Klabu ya Mtibwa Sugar, Dickson Job, amesaini mkataba wa miaka miwili na nusu wa kuitumikia Klabu ya Yanga iliyopo chini ya kocha Mrundi Cedric Kaze.

Kwa muda sasa Job ambaye ni chaguo la kwanza katika kikosi cha Mtibwa Sugar, amekuwa akihusishwa na kujiunga na Yanga, na jana rasmi alisaini mkataba wa miaka miwili na nusu wa kuitumikia klabu hiyo iliyopo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya utambulisho wa beki huyo katika mtandao rasmi wa klabu hiyo, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema tayari wamemalizana na Job pamoja na klabu yake baada ya kumnunua mchezaji huyo.

"Sisi huwa tunanunua wachezaji, na Job tayari muda mchache uliopita (saa 8:32), tumeshamwingiza kwenye 'system' ya usajili ya TFF, unajua kumsajili mchezaji ni moja na pili ni kumuingiza katika system ya TFF (Shirikisho la Soka nchini) ili uweze kumtumia," alisema Bumbuli.

Alisema Job atajiunga na timu hiyo na kuanza kuitumikia baada ya kupona majeraha aliyoyapata hivi karibuni ambayo yalimsababishia kuenguliwa katika kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars kinachojiandaa na michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

"Ana majeraha madogo si makubwa sana, hivyo atakapopona moja kwa moja atajiunga na timu kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu na michuano mingine," alisema.

Kuhusu usajili wa klabu hiyo kwa ujumla katika dirisha hili dogo linalotarajiwa kufungwa Januari 15, mwaka huu saa sita usiku, Bumbuli alisema bado kuna nafasi moja ya mshambuliaji kutoka nje ambaye watamtangaza baada ya Sikukuu za Mapinduzi, zinazoadhimishwa leo visiwani Zanzibar.

"Kuna mshambuliaji mmoja kutoka nje, lakini siwezi kukutajia wala nchi anayotoka maana hiyo tunataka iwe 'sapraizi' na zawadi kwa mashabiki wetu katika sherehe hizi za Mapinduzi," alisema.

# Kocha Malindi asifu kuimarika Mapinduzi

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa timu ya Malindi, Mohammed Bandru, amesema licha ya kutosonga mbele kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, lakini imekuwa kipimo tosha kwa timu za Zanzibar kuboresha viwango vyao.

Kauli hiyo aliitoa baada ya kutolewa katika michuano hiyo kwa kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Azam FC juzi usiku, bao pekee likifungwa na Agrey Morris kwa mkwaju wa penalti.

Mohammed alisema msimu huu timu za Zanzibar zimekuwa na mabadiliko makubwa kwa kupata fursa ya kupambana na timu bora kutoka Bara baada ya kutofungwa mabao mengi.

Alisema makundi ambayo timu za Bara na Zanzibar zilikutana, walilazimika kufungwa bao 1-0, kutoka suluhu ama sare ya mabao.

"Ukiangalia misimu iliyopita, timu za Zanzibar zilikuwa tofauti na msimu huu hakuna timu kutoka Bara ambayo imetufunga idadi kubwa ya mabao, ukitazama mechi yetu dhidi ya Azam FC wametutoa kwa kutufunga kwa penalti.

"Hii inaonyesha jinsi ambavyo timu za hana nyumbani zilivyoimarika na kuleta ushindani mkubwa kwa timu za Bara," alisema Mohammed.

# Malale atoa angalizo vitambi Polisi Tanzania

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Polisi Tanzania limetoa angalizo kwa wachezaji wake katika kipindi hiki cha mapumziko ya Ligi Kuu kuhakikisha hawalei vitambi.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka visiwani Zanzibar, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Malale Hamsini, alisema mchezaji ambaye atarudi na uzito mkubwa ama kitambi hatampa nafasi ya kucheza.

"Nimewapa wachezaji mapumziko ya siku 10 mpaka tarehe 16 ndio tutaanza tena kambi kwa ajili ya kujiandaa na raundi ijayo ya Ligi Kuu, lakini nimewataka kuhakikisha hawaongezeki uzito.

"Tunaendelea na mazungumzo mazuri na viongozi si ya kuvunja mkataba bali ni yakuleta mafanikio katika klabu," alisema.

Kwa upande wa msemaji wa klabu hiyo, Frank Lukwaro, alisema hawana mpango wa kuachana na kocha huyo huku akieleza kusikitishwa na taarifa zinazozagaa kuwa wameachana naye.

# Michezo

Jumanne Januari 12, 2021

Nipashe




## SANCHO CHAMBO YA HAALAND CITY

HABARI UK 22

LA USIKU...



Beki wa Sassuolo (chini), akiucheza mpira dhidi ya mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo, kwenye mechi ya Serie A iliyopigwa Turin juzi na Juve kushinda 3-1 huku straika huyo akihitimisha ushindi huo kwa bao la 'usiku' (dakika za majeruhi). **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, YANGA NDIYO HIVYO MAPINDUZI CUP

●●●Azam FC yatupwa nje kwa penalti mapema, fainali yasubiriwa kwa hamu kesho, lakini...

**Na Adam Fungamwango**

KIPA wa Yanga, Farouk Shikalo, jana jioni alikuwa shujaa, baada ya kupangua penalti mbili za wachezaji wa Azam FC kwenye Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar na kuiwezesha timu yake kutinga fainali ya Kombe la Mapinduzi, itakayochezwa kesho Jumatano.

Kutangulia kwa Yanga fainali kuliamsha nderemo huku kila kona uwanjani hapo mashabiki wakiiombea Simba kuichapa Namungo FC katika nusu fainali ya pili jana usiku ili washuhudie 'dabi' ya watani hao wa jadi kwenye Kombe la Mapinduzi katika Uwanja wa Amaan.

Shikalo, raia wa Kenya, alipangua penalti za Awesu Awesu na Daniel Amoah na kuifanya Yanga kushinda kwa penalti 5-4.

Timu hizo zilitinga katika changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya mechi hiyo ya nusu fainali kumalizika kwa sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90 za mchezo.

Kipa wa Azam FC, Benedict Haule, ambaye aliingia dakika za majeruhi, maalum kwa ajili ya kukaa langoni wakati wa mikwaju ya penalti, aliambulia kuokoa penalti moja tu ya Michael Sarpong.

Penalti za Yanga zilikwamishwa wavuni na Tuisila Kisinda, Mukoko Tonombe, Paul Geofrey, Abdallah Shaibu 'Ninja' na Zawadi Mauya, huku zile za Azam zikiwekwa wavuni na Bruce Kangwa, Ally Niyonzima, Mudathir Yahaya, na Nicolaus Wadada.

Na kwa upande wa mabao ya timu hizo kwenye dakika 90, yalifungwa kipindi cha pili dakika ya 51, Yanga ikitangulia kwa bao lililofungwa na Kisinda, baada ya mpira mrefu uliopigwa kutoka nyuma, akiwazidi kasi mabeki wa Azam, kabla ya kuubetua na kujaa wavuni na kumuacha kipa Wilbol Maseke akidaka ardhi.

Straika wa zamani wa Yanga, Obrey Chirwa, alisawazisha bao hilo dakika ya 66, baada ya krosi safi kutoka kwa Kangwa na kupigwa kichwa cha kuparaza, mpira ukawachanganya kipa Shikalo na aliyekuwa sambamba na Mukoko, na kujaa wavuni.

Dakika ya pili tu ya mchezo, Azam ilipiga hodi langoni mwa Yanga kwa Never Tegere kuambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto kabla ya kuachia shuti kali, lililopanguliwa na kipa Farouk Shikalo na kuwa kona ambayo pia ilizua kizaazaa kwenye lango la Yanga kutokana na kuunganishwa tena na Tegere, lakini mabeki walikaa imara na kuokoa hatari hiyo.

Yanga ilifanya shambulizi la hatari langoni mwa Azam dakika 12 baadaye, wakati Tuisila Kisinda alipoingia kwenye eneo la hatari la Azam na kupiga shuti, lakini lilimbabatiza mchezaji mwenzake Kibwana Shomari na kutoka nje ya lango.

Kwa matokeo hayo, ndivyo tena Yanga ilikuwa ikisubiri mshindi kati ya Simba na Namungo ili kujua itakutana na nani fainali ya hapo kesho.

## TSHISHIMBI: NI VITA SIMBA, AS VITA CAF

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa zamani wa Yanga, Papy Tshishimbi, anaichezea AS Vita ya kwao DR Congo kwa sasa, amesema mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Simba, haitakuwa rahisi kwa upande wowote, timu hizo zitakapokutana mwezi ujao.

Simba mbali na AS Vita, timu hizo zipo Kundi A na Al-Merrikh ya Sudan pamoja na mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Al Ahly ya Misri.

Hata hivyo, katika michuano hiyo mwaka 2018, Simba ilikubali kipigo cha mabao 5-0 ugenini dhidi ya Al Ahly na AS Vita, kabla ya kujibu mapigo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kuzichapa 1-0 na 2-1, hivyo kutinga robo fainali pamoja na mabingwa watetezi hao.

Lakini Tshishimbi akizungumza na mwandishi wetu kuelekea mechi hiyo dhidi ya Simba nchini DR Congo Februari 12, mwaka huu, alisema ni ngumu na wao hawautazami mchezo huo pekee bali timu zote katika kundi hilo.

**"Naifuatilia sana Simba, kwa sasa ipo katika michuano ya Mapinduzi, najua ni timu nzuri na inafanya vizuri, lakini kocha ametutaka kutoangalia mechi na Simba pekee, bali zote tulizopangwa nazo katika kundi letu," alisema mchezaji huyo ambaye aliachana na Yanga baada ya kushindwana dau la kuongeza mkataba mpya.**

Tshishimbi alisema kocha wao, Florent Ibenge, amewataka kuweka malengo ya kushinda mechi zote ili kuongoza kundi lao na kusonga mbele katika michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002